Disclaimer : Ministry of Finance and Planning repository shall be regarded as a publisher and bears no liability for any damage upon using contents of the repository.

Budget Documents Budget Guidelines

2018

Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali wa Mwaka 2019-20 / 2021-22

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Wizara ya Fedha na Mipango

https://repository.mof.go.tz/handle/123456789/398

Downloaded from Ministry of Finance and Planning Repository

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO

MWONGOZO WA MAANDALIZI YA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2019/20 – 2021/22

OKTOBA, 2018

SEHEMU YA KWANZA

SERA NA MFUMO WA BAJETI KATIKA KIPINDI CHA MUDA WA KATI

YALIYOMO

SEHEMU YA KWANZA iii
SERA NA MFUMO WA BAJETI KATIKA KIPINDI CHA MUDA WA KATI..... iii

SURA YA KWANZA 1
MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MWAKA 2017/18 1
1.1. Utangulizi 1
1.2. Utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka 2017/18 1
1.2.1. Mapato ya Ndani 1
1.2.2. Matumizi 1
1.2.3. Ugharamiaji wa Nakisi ya Bajeti 2
1.3. Mapitio ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Baadhi ya Sekta na Miradi ya Kimkakati 3

SURA YA PILI 9
MAPITIO YA MWENENDO NA MWELEKEO WA UCHUMI KATIKA KIPINDI CHA MUDA WA KATI 9
2.1. Utangulizi 9
2.2. Mwenendo wa Hali ya Uchumi 9
2.2.1. Mapitio ya Takwimu za Pato la Taifa Kufuatia Mabadiliko ya Mwaka wa Kizio kutoka 2007 kuwa 2015 9
2.2.2. Ukuaji wa Pato la Taifa 9
2.2.3. Mwenendo wa Mfumuko wa Bei 10
2.2.4. Mfumuko wa Bei kwa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki 11
2.2.5. Ujazi wa Fedha na Karadha 11
2.2.6. Mwenendo wa Viwango vya Ubadilishaji Fedha 14
2.2.7. Mwenendo wa Sekta ya Benki 15
2.2.8. Deni la Taifa 16
2.2.9. Mwenendo wa Sekta ya Nje 17
2.3. Mwelekeo wa Uchumi Jumla na Maoteo ya Muda wa Kati 18
2.3.1. Mwelekeo wa Ukuaji wa Uchumi Duniani 18
2.3.2. Maoteo ya Ukuaji wa Pato la Taifa katika Kipindi cha Muda wa Kati 19
2.3.3. Maoteo ya Ukuaji Kisekta 20
2.3.4. Mfumuko wa Bei Katika Kipindi cha Muda wa Kati 21
2.3.5. Sera ya Fedha 22
2.3.6. Sekta ya Nje 22

SURA YA TATU 24

MPANGO NA BAJETI KWA MUDA WA KATI 24
3.1. Utangulizi 24
3.2. Sera za Mapato na Makadirio 24
3.2.1. Sera za Mapato ya Ndani 24
3.2.2. Makadirio ya Mapato ya Ndani 24
3.3. Sera za Matumizi na Makadirio 27
3.3.1. Sera za Matumizi 27
3.3.2. Makadirio ya Matumizi 27
3.3.3. Uainishaji wa Makadirio ya Matumizi Kiuchumi (2019/20 – 2021/22) 28
3.3.4. Uainishaji wa Makadirio ya Matumizi Kulingana na Majukumu ya Serikali (CoFoG) (2019/20 – 2021/22) 30
3.3.5. Misaada na Mikopo 30
3.3.6. Ukopaji kutoka Vyanzo vya Ndani 31
3.3.7. Ukopaji kutoka Vyanzo vya Nje 32
3.3.8. Makadirio ya Kuziba Nakisi ya Bajeti 32
3.4. Vipaumbele katika Kipindi cha Muda wa Kati 36
3.4.1. Kukuza Uchumi na Ujenzi wa Msingi wa Uchumi wa Viwanda 36
3.4.2. Maendeleo ya Watu 36
3.4.3. Kuboresha Mazingira ya kufanya Biashara na Uwekezaji 37
3.4.4. Kuboresha Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano 37

SURA YA NNE 38
VIHATARISHI VYA KIBAJETI KATIKA MUDA WA KATI 38
4.1. Utangulizi 38
4.2. Maeneo ya Vihatarishi 38
4.3. Hatua za Kukabiliana na Vihatarishi 40

Kiambatisho I:Overview of Expenditure by Divisions and Groups of CoFOG 43

Kiambatisho II:TAARIFA YA UKUSANYAJI WA MADUHULI KWA WIZARA/IDARA KWA MWAKA 2017/18 45

Kiambatisho III:UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MWAKA 2017/18 KWA MAFUNGU 46

SEHEMU YA PILI 49
MWONGOZO WA MAANDALIZI YA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2019/20 – 2021/22 49

SURA YA KWANZA 51
MWONGOZO WA MAANDALIZI YA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2019/20 – 2021/22 51
1.1. Mfumo wa Mapato na Matumizi 51
1.1.1. Mapato ya Serikali 51
1.1.2. Matumizi ya Serikali 51
1.2. Uandaaji wa Mipango na Bajeti 52
1.2.1. Kamati za Bajeti 52
1.2.2. Ratiba ya Maandalizi ya Mipango na Bajeti 52
1.2.3. Uchambuzi wa Mipango na Bajeti 52
1.2.4. Majumuisho ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali 54
1.2.5. Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi-PPP 54
1.2.6. Uingizaji wa Takwimu za Bajeti ya Serikali kwenye Mifumo ya CBMS na PlanRep 54
1.3. Mambo Mengine ya Kuzingatiwa katika Uandaaji wa Mipango na Bajeti 55
1.4. Maelekezo Mahususi kwa Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. 59
1.4.1. Maelekezo kwa Sekretarieti za Mikoa 59
1.4.2. Maelekezo Mahsusi kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa 60
1.5. Ufuatiliaji, Tathmini na Utoaji Taarifa za Utekelezaji 65
1.5.1. Ufuatiliaji na Tathmini 65
1.5.2. Utoaji Taarifa za Utekelezaji 65
1.6. Hitimisho 66

SURA YA PILI 67
UTARATIBU WA UWASILISHAJI WA MPANGO NA BAJETI, UTEKELEZAJI NA UTOAJI WA TAARIFA 67
2.1. Utangulizi 67
2.2. Maandalizi ya Mpango na Bajeti 67
2.3. Utekelezaji wa Bajeti 68
2.4. Taarifa za Utekelezaji 69

SURA YA KWANZA

MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MWAKA 2017/18

1.1. Utangulizi

1. Sura hii inaeleza kwa ufupi utekelezaji wa Serikali katika mapato, matumizi, misaada na mikopo kwa mwaka 2017/18. Tathmini imefanyika kwa kulinganisha utekelezaji dhidi ya malengo katika kipindi husika. Kadhalika, mapitio yamefanyika kwa miradi michache inayoendelea na mipango mingine ya Serikali kwa kulinganisha matumizi halisi dhidi ya malengo yaliyowekwa pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika kipindi hicho.

1.2. Utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka 2017/18

2. Katika mwaka 2017/18, Serikali ilichukua hatua mbalimbali za kisera na kiutawala ili kuongeza ukusanyaji wa mapato ya ndani. Hatua hizo ni pamoja na: kuimarisha usimamizi wa kodi; kudhibiti uvujaji wa mapato kwenye vyanzo vilivyopo vya kodi; kupanua wigo wa kodi; kuongeza matumizi ya TEHAMA katika usimamizi wa kodi; na kuimarisha matumizi ya Mfumo wa Kielektroniki wa Ukusanyaji wa Mapato ya Serikali (GePG). Kwa upande mwingine, Sera za Matumizi zililenga katika kuwianisha mapato na vipaumbele vya matumizi kupitia usimamizi wa Sheria ya Bajeti, SURA 439. Utekelezaji wa bajeti unaelezwa katika vifungu vifuatavyo:

1.2.1. Mapato ya Ndani

3. Katika mwaka 2017/18, Shilingi bilioni 17,944.9 zilikusanywa sawa na asilimia 90 ya makadirio ya Shilingi bilioni 19,977.0. Kati ya mapato hayo, mapato ya kodi ni Shilingi bilioni 15,191.0 sawa na asilimia 89 ya makadirio ya Shilingi bilioni 17,106.3, mapato yasiyo ya kodi ni Shilingi bilioni 2,212.4 sawa na asilimia 101 ya makadirio ya Shilingi bilioni 2,183.4 na mapato ya ndani ya Serikali za Mitaa ni Shilingi bilioni 541.5 sawa na asilimia 79 ya makadirio ya Shilingi bilioni 687.3. Mapato yaliyokusanywa yaliongezeka kwa asilimia 7 ikilinganishwa na mapato ya Shilingi bilioni 16,639.8 yaliyokusanywa katika kipindi kama hicho mwaka 2016/17. Ongezeko hilo limetokana na juhudi za Serikali ya Awamu ya Tano katika kuchukua hatua za kuimarisha usimamizi wa makusanyo ya mapato.

1.2.2. Matumizi

4. Katika mwaka 2017/18, matumizi ya Serikali yalifikia Shilingi bilioni 25,321.7 sawa na asilimia 80 ya makadirio ya Shilingi bilioni 31,711.9. Kati ya kiasi hicho, Shilingi bilioni 18,778.5 kilikuwa ni Matumizi ya Kawaida sawa na asilimia 93 ya makadirio ya Shilingi bilioni 20,279.3 na Shilingi bilioni 6,543.2 zilikuwa ni Matumizi

ya Maendeleo sawa na asilimia 57 ya makadirio ya Shilingi bilioni 11,432.7.

(a) Matumizi ya Kawaida

5. Matumizi ya Kawaida yanajumuisha Mishahara, malipo ya Deni la Serikali na Matumizi Mengineyo. Katika mwaka 2017/18, Matumizi ya Kawaida yalikuwa Shilingi bilioni 18,778.5 sawa na asilimia 92.6 ya makadirio. Kati ya kiasi hicho, Mishahara ni Shilingi bilioni 6,338.1 sawa na asilimia 88 ya makadirio ya Shilingi bilioni 7,205.8, Malipo ya Deni la Serikali ni Shilingi bilioni 8,133.1 sawa na asilimia 99.9 ya makadirio ya Shilingi bilioni 8,140.4 na Matumizi Mengineyo yalikuwa Shilingi bilioni 4,307.3 sawa na asilimia 92 ya makadirio.

(b) Matumizi ya Maendeleo

6. Katika mwaka 2017/18, Matumizi ya Maendeleo yalikuwa Shilingi bilioni 6,543.2 sawa na asilimia 57 ya makadirio ya Shilingi bilioni 11,432.7. Kati ya matumizi hayo, fedha za ndani ni Shilingi bilioni 5,068.8 sawa na asilimia 62 ya makadirio ya shilingi bilioni 8,179.1 na fedha za nje ni Shilingi bilioni 1,474.4 sawa na asilimia 49 ya makadirio ya Shilingi bilioni 3,029.8. Matumizi ya fedha za nje hayajumuishi baadhi ya fedha kutoka kwa Washirika wa Maendeleo zilizopelekwa moja kwa moja kwenye utekelezaji wa miradi ambazo hazikupita kwenye mfumo wa malipo wa Serikali. Fedha hizi zitajumuishwa pindi taratibu za kiuhasibu zitakapo kamilika.

1.2.3. Ugharamiaji wa Nakisi ya Bajeti

(a) Misaada na Mikopo Nafuu

7. Katika mwaka 2017/18, fedha zilizopokelewa zilikuwa Shilingi bilioni 2,466.0 sawa na asilimia 62 ya miadi ya fedha za nje (Shilingi bilioni 3,971.1). Fedha za Misaada ya Kibajeti zilizotolewa zilifikia Shilingi bilioni 247.3 (sawa na asilimia 26 ya makadirio ya Shilingi bilioni 941.3), Mifuko ya Kisekta zilikuwa Shilingi bilioni 188.2 (sawa na asilimia 34 ya makadirio ya Shilingi bilioni 556.1) na fedha za Miradi ya Maendeleo zilikuwa Shilingi bilioni 2,030.5 (sawa na asilimia 82 ya makadirio ya Shilingi bilioni 2,473.8). Kutofikiwa kwa lengo la kupokea fedha za Misaada ya Kibajeti pamoja na Mifuko ya Kisekta kulitokana na; kuchelewa kuwasilishwa kwa taarifa ya vigezo vya utekelezaji wa Sera za Maendeleo (DPOs) iliyopelekea kuongezeka kwa muda wa majadiliano na kutiliana saini katika programu mpya ya utoaji wa fedha za Misaada ya Kibajeti kwa miaka mitatu (2017-2019). Aidha, makubaliano kati ya Serikali na Benki ya Dunia kuhusu viashiria vya utoaji wa fedha kwenye sekta ya nishati yalichukua muda mrefu.

8. Katika kuimarisha ushirikiano baina ya Serikali na Washirika wa Maendeleo, Serikali iliridhia Mwongozo wa Ushirikiano wa Maendeleo Tanzania na Mpango

Kazi wake. Mwongozo huo utawezesha kuwa na majadiliano yatakayoimarisha uhakika wa upatikanaji wa fedha za nje. Aidha, Mwongozo unasisitiza kuheshimu makubaliano ya ushirikiano ikijumuisha uhakika wa miadi ya Misaada ya Kibajeti. Hatua hizi zililenga kuwa na bajeti endelevu, pamoja na kuhakikisha upatikanaji wa rasilimali fedha katika kipindi cha muda wa kati.

(b) Mikopo yenye Masharti ya Kibiashara

9. Katika mwaka 2017/18, Serikali ilikopa Shilingi bilioni 7,055.8 (sawa na asilimia 90.9) ya Shilingi bilioni 7,763.9. Kati ya mikopo hiyo, Shilingi bilioni 1,351.5 zinatokana na vyanzo vya nje na Shilingi bilioni 5,704.4 ni vyanzo vya masoko ya ndani. Kati ya mikopo ya ndani, Shilingi bilioni 4,835.2 ni malipo ya mtaji wa deni la ndani (rollover) na Shilingi bilioni 869.2 ni mikopo mipya kwa ajili ya kugharimia bajeti ya Maendeleo.

1.3. Mapitio ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Baadhi ya Sekta na Miradi ya Kimkakati

10. Sehemu hii inaelezea miradi ya kimkakati na programu mahsusi zinazotekelezwa kama ilivyoainishwa kwenye Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2016/17 – 2020/21) yenye lengo la kuchochea mageuzi ya viwanda kwa maendeleo ya uchumi na watu. Miradi hiyo inatekelezwa katika sekta za: Kilimo, Usafiri, Afya, Elimu, Maji na Nishati.

11. **Kilimo, Mifugo na Uvuvi:** katika kutambua mchango wa sekta ya kilimo katika kupunguza umaskini, Serikali ililenga: kuongeza uzalishaji katika kilimo, mifugo na uvuvi; kuongeza thamani na kuboresha shughuli za Kilimo kupitia mafunzo, utoaji wa pembejeo na huduma za ugani. Mafanikio yaliyopatikana katika sekta hii kwa mwaka 2017/18 ni pamoja na:

(i) **Uzinduzi wa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo Awamu ya II**: inalenga kufanya mapinduzi katika sekta ya kilimo (mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi) kwa kuongeza tija, kufanya kilimo kiwe cha kibiashara na kuboresha kipato na maisha kwa wakulima wadogo, usalama wa chakula na lishe;

(ii) **Uimarishaji wa Upatikanaji wa Pembejeo**: upatikanaji wa mbegu bora uliongezeka na kufikia tani 51,700.5 mwaka 2017/18 kutoka tani 36,482 mwaka 2015/16, na tani 435,178 za mbolea zilinunuliwa na kusambazwa katika mwaka 2017/18 ikilinganishwa na tani 302,450 zilizonunuliwa katika mwaka 2015/16.

(iii) **Uimarishaji wa Ushirika na Masoko ya Mazao**: Serikali iliendelea

kuimarisha mifumo ya masoko na Ushirika ikiwa ni pamoja na kujumuisha mazao matano ya kimkakati (korosho, tumbaku, kahawa, chai na pamba) katika mfumo huo. Juhudi hizo ziliwezesha Vyama vya Ushirika kuongezeka kutoka 7,888 mwaka 2015 hadi 10,990 mwaka 2017. Aidha, juhudi za Serikali katika kuimarisha Mfumo wa Stakabadhi Ghalani ziliwezesha kuongezeka kwa bei za mazao (**korosho** kutoka Shilingi 2,500 mwaka 2016/17 hadi Shilingi 4,100 kwa kilo mwaka 2017/18; **Chai** kutoka Shilingi 251 hadi 314 kwa kilo ya majani mabichi yanayouzwa kiwandani; **Katani** kutoka Shilingi milioni 2.2 mwaka 2015/16 hadi Shilingi milioni 3.3 kwa tani mwaka 2017/18; na **Ufuta** kutoka Shilingi 1,200 mwaka 2015/16 hadi Shilingi 3,770 kwa kilo mwaka 2017/18);

(iv) Ujenzi wa mabwawa mawili ya mifugo ya Olyapasei (Kiteto) na Kwamaliga (Kilindi) pamoja na lambo la Masusu katika Wilaya ya Ngorongoro;

(v) Kuzalisha na kusambaza dozi 28,427,100 za chanjo ya ugonjwa wa Mdondo, dozi 882,100 za chanjo ya ugonjwa wa Kimeta, dozi 128, 600 za chanjo ya ugonjwa wa Chambavu na dozi 625 za chanjo ya ugonjwa wa Kutupa Mimba; na

(vi) **Hifadhi ya Chakula:** katika mwaka 2017/18, Serikali kupitia Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) ilinunua tani 26,038.6 za mahindi ili kuwa na uhakika wa Chakula nchini. Aidha, katika kipindi hicho Serikali ilikamilisha ukarabati wa maghala 105 yenye uwezo wa kuhifadhi tani 31,500.

12. **Ujenzi wa Reli katika Kiwango cha *Standard Gauge*:** Utekelezaji wa awamu ya kwanza ya mradi kutoka Dar es Salaam hadi Morogoro (km 300) umefikia asilimia 24. Kazi zilizofanyika ni pamoja na ujenzi wa njia kwa ajili ya kuhudumia mradi (kupitisha watu, mitambo na vifaa vya ujenzi); usanifu wa stesheni na majengo; utengenezaji wa mataruma; upimaji wa ardhi kwa ajili ya njia ya reli; na ujenzi wa madaraja na tuta la reli. Kiasi cha fedha kilichotolewa kwa mwaka 2017/18 kilikuwa Shilingi bilioni 900.0, sawa na asilimia 100 ya bajeti. Awamu ya pili inayohusisha ujenzi wa reli kutoka Morogoro hadi Makutupora, Dodoma (km 422) inaendelea. Kazi zinazoendelea kufanyika ni pamoja na utwaaji wa ardhi kutoka kwa wananchi, uletaji wa vifaa vya ujenzi, na usanifu wa mwelekeo wa njia.

13. **Mradi wa Kufua Umeme MW 2,100 wa Rufiji:** kwa mwaka 2017/18, Serikali iliendelea na ukamilishwaji wa miundombinu wezeshi kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa Kufua Umeme katika mto Rufiji utakao kuwa na uwezo wa kuzalisha Megawati 2,100 za umeme. Kazi zinazoendelea ni pamoja na ujenzi wa njia ya

kusambaza umeme wa kV 33 kutoka Dakawa (*Morogoro*) hadi eneo la mradi na taratibu za zabuni kwa ajili ya kumpata Mkandarasi wa mradi zinaendelea.

14. **Usambazaji wa Umeme Vijijini:** katika mwaka 2017/18, Shilingi bilioni 295.0 sawa na asilimia 81 ya makadirio ya Shilingi bilioni 362.5 zilitumika. Jumla ya vijiji 557 vimeunganishiwa umeme kupitia Mpango wa Mradi wa Kusambaza Umeme Vijijini Awamu ya Tatu (REA Phase III). Hadi kufikia mwezi Agosti, 2018, mradi umewezesha taasisi 903, shule 1,983, maeneo ya biashara 1,743 na maabara za tiba 19 kuunganishwa umeme.

15. Ujenzi wa Jengo la Tatu la Abiria katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere: katika mwaka 2017/18, Shilingi bilioni 169.3 zilitumika ambapo utekelezaji umefikia asilimia 78 na unatarajiwa kukamilika Mei 2019. Kazi zilizokamilika ni pamoja na; Ujenzi wa eneo la maegesho ya ndege na viungio vyake lenye ukubwa wa mita za mraba 227,000 ambalo lina uwezo wa kuegesha ndege 30 kwa wakati mmoja; Usimikaji wa "escalators" tisa (9), "travelator" mbili (2) na madaraja 13 ya kupanda na kushuka kwenye ndege; Ujenzi wa eneo la maegesho ya magari lenye uwezo wa kuegesha magari 2,075 kwa wakati mmoja; Ujenzi wa barabara za kuingia na kutoka eneo la jengo zenye urefu wa kilometa 1.8; Ujenzi wa Uzio wa kuzunguka uwanja kwa ajili ya usalama na miundombinu ya maji safi na majitaka. Kazi nyingine zilizokamilika ni pamoja na: ujenzi wa tanki la maji lenye ujazo wa lita milioni 2.26; ujenzi wa kituo kikubwa cha umeme chenye uwezo wa kV 33; usimikaji wa lifti 14 na jenereta (2,000 kVA) saba (7) za kufua na kusambaza umeme kwenye eneo la jengo; ujenzi wa mifumo ya kujaza mafuta kwenye ndege; na kusimika mifumo yote ya mawasiliano na usalama kwenye jengo.

16. **Kuimarisha Shirika la Ndege Tanzania**: Serikali imeendelea na juhudi za kuimarisha Shirika la Ndege ili kuboresha huduma za usafiri wa anga ndani na nje ya nchi. Katika mwaka 2017/18, ndege moja aina ya Bombardier Q400 yenye uwezo wa kubeba abiria 76 na nyingine ni aina ya Dreamliner–Boeing 787–8 yenye uwezo wa kubeba abiria 262 zimenunuliwa na kuanza kutumika. Ndege hizi zitaongeza ufanisi katika uendeshaji wa ATCL na kuwezesha upatikanaji wa huduma za uhakika na nafuu za usafiri wa anga nchini. Vile vile, safari za moja kwa moja za kimataifa zitapunguza gharama za usafiri na hivyo kuongeza idadi ya watalii wanaowasili na kuongeza mchango wa sekta ya utalii katika ukuaji wa uchumi.

17. **Maji:** katika mwaka 2017/18, Shilingi bilioni 150.3 sawa na asilimia 95 ya makadirio ya Shilingi bilioni 158.5 zilitolewa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maji mijini na vijijini kupitia Mfuko wa Maji. Fedha hizo zilielekezwa kwenye miradi ya maji katika Halmashauri 59, Mamlaka za Maji 19 na miradi 24

inayosimamiwa na Wizara ya Maji na Umwagiliaji katika mikoa. Vilevile, jumla ya miradi 1,493 ya maji vijijini imekamilika na kuwanufaisha wananchi 21,321,500 nchi nzima.

18. **Madini:** kufanya mapitio ya Sheria za Madini ili nchi inufaike zaidi katika rasilimali hiyo; ujenzi wa ukuta mkubwa wenye mzingo wa km 24.5 kuzunguka migodi ya Tanzanite Mirerani; kuongezeka kwa makusanyo ya maduhuli yatokanayo na madini kufikia Shilingi bilioni 301.2 mwaka 2017/18 ikilinganishwa na lengo la Shilingi bilioni 194.4; kukamilika kwa kituo cha mfano cha umahiri cha Rwamgasa Mkoani Geita kwa ajili ya mafunzo ya wachimbaji wadogo; Kuendelea na ujenzi wa vituo 7 vya umahiri katika vituo vya Bariadi, Musoma, Bukoba, Mpanda, Chunya, Songea na Handeni kwa ajili ya mafunzo ya wachimbaji wadogo; na kuanzisha utaratibu wa wamiliki wa leseni za madini kutumia huduma na bidhaa za ndani (local content) ili kuwapatia wananchi fursa za ajira.

19. **Elimu Msingi Bila Ada:** Serikali imeendelea kutekeleza sera ya utoaji elimu msingi bila ada ambapo katika mwaka 2017/18 Shilingi bilioni 249.6 zilitolewa. Utekelezaji huo umechangia kuongezeka kwa uandikishaji wa wanafunzi katika darasa la kwanza kutoka wanafunzi 1,568,378 mwaka 2015 hadi wanafunzi 2,078,379 mwaka 2018. Vile vile, uandikishaji wanafunzi kwa upande wa Sekondari umeongezeka kutoka wanafunzi 448,826 mwaka 2015 hadi wanafunzi 562,695 wa kidato cha kwanza mwaka 2017. Ongezeko hilo la wanafunzi, limepelekea kuongezeka kwa Shule za Msingi kutoka 17,174 mwaka 2016 hadi 17,596 mwaka 2017 na Shule za Sekondari kutoka 4,759 mwaka 2016 hadi 5,196 mwaka 2017.

20. **Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu:** Katika mwaka 2017/18, wanafunzi walionufaika na mikopo ya elimu ya juu walifikia 122,623 ikilinganishwa na wanafunzi 116,205 mwaka 2016/17. Matumizi kwa ajili ya mikopo katika mwaka 2017/18 yalikuwa Shilingi bilioni 443.1 ukilinganisha na Shilingi bilioni 495.4 mwaka 2016/17. Kupungua kwa fedha za mikopo ya wanafunzi kunatokana na kuboreshwa kwa mifumo ya udahili na vigezo vya utoaji mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu, kufutwa kwa baadhi ya Vyuo Vikuu, kufutwa kwa baadhi ya Kozi na mapitio mapya ya vigezo vya utoaji mikopo.

21. **Ukarabati wa Shule Kongwe za Sekondari na Ujenzi wa Nyumba za Walimu**: katika mwaka 2017/18, Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA) ilikamilisha miradi mbalimbali ikijumuisha: ukarabati wa majengo ya shule kongwe 10 za sekondari ambapo Shilingi bilioni 18.7 zilitumika; ujenzi wa nyumba 70 za walimu katika shule za sekondari zilizopo kwenye maeneo yasiyofikika kiurahisi na ya pembezoni ambapo Shilingi bilioni 4.2 zilitumika; utoaji wa ruzuku ya Shilingi

bilioni 3.1 kwenye Vyuo Vikuu na shule za sekondari kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia ikiwa ni pamoja na ujenzi wa miundombinu na utoaji elimu inayolenga kuleta usawa katika utoaji wa elimu.

22. **Afya:** Mafanikio yaliyopatikana katika kuboresha huduma za afya nchini ni kama ifuatavyo:

(i) Kuongezeka kwa bajeti ya dawa kutoka Shilingi bilioni 31 mwaka 2015/16 hadi kufikia bilioni 270 mwaka 2018/19 na hivyo kuongeza upatikanaji wa dawa muhimu katika vituo vya kutolea huduma za afya nchini kutoka asilimia 35 mwaka 2015 asilimia 89.6 mwaka 2018/19. Vile vile, mfumo wa kusambaza dawa kutoka Bohari ya Dawa hadi vituo vya kutolea huduma za Afya umeimarishwa baada ya Serikali kununua magari 181 kwa ajili ya usambazaji wa dawa;

(ii) Kuimarisha huduma za Matibabu ya Kibingwa kwa kuboresha miundombinu ya kutolea huduma, ununuzi wa vifaa tiba vya kisasa na hivyo kupunguza rufaa za wagonjwa nje ya nchi kutoka wagonjwa 553 mwaka 2015 mpaka kufikia wagonjwa 103 mwaka 2018. Aidha, kati ya Julai 2017 hadi Oktoba 2018, jumla ya wagonjwa 28 walipatiwa huduma ya kupandikiza figo hivyo kupunguza gharama kwa wastani kutoka shilingi milioni 100 hadi shilingi milioni 20 kwa mgonjwa mmoja endapo angepelekwa nje ya nchi. Vile vile, jumla ya Watoto 11 wamepandikizwa vifaa vya kusikia (Cochlear Implant) hivyo kuokoa milioni 64 kwa mtoto mmoja endapo angepata huduma hii nje ya nchi;

(iii) Kuimarishwa kwa huduma za Kibingwa za moyo katika Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI), ambapo kwa mwaka 2017/18, wagonjwa 770 walifanyiwa upasuaji wa tundu dogo bila kufungua kifua ikilinganishwa na wagonjwa 276 mwaka 2016/17. Aidha, wagonjwa waliofanyiwa upasuaji wa kufungua kifua mwaka 2017/18 ni 275 ikilinganishwa na wagonjwa 130 mwaka 2015/16;

(iv) Kuendelea kuboresha huduma za Kibingwa za Tiba ya Saratani ambapo Taasisi ya Saratani Ocean Road imenunua mashine mbili (2) mpya za mionzi na za kisasa. Hali hiyo imechangia kupunguza muda wa mgonjwa mpya wa saratani kusubiri kuanza tiba ya mionzi kutoka wiki 6 hadi wiki 2. Vile vile, upatikanaji wa dawa katika Taasisi hiyo umeimarika kutoka asilimia 4 mwaka 2015 hadi kufikia asilimia 85 Julai 2018;

(v) Kuimarisha miundombinu ya vituo vya afya 210 kwa kuvijengea vyumba vya upasuaji, wodi za wazazi, maabara na nyumba za watumishi ili kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi. Hatua hii imewezesha kuongezeka kwa vituo vya kutolea huduma za uzazi kutoka vituo 117 mwaka 2015 hadi vituo 327;

(vi) Kuendelea kutekeleza mikakati ya kutokomeza UKIMWI. Maambukizi

kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto yamepungua kutoka asilimia 7.6 mwaka 2015 hadi asilimia 4.8;

(vii) Katika mwaka 2015/16 hadi 2017/18 Maambukizi ya Malaria yamepungua kutoka asilimia 14 hadi kufikia asilimia 7, aidha katika kukabiliana na maambukizi ya Malaria Serikali imegawa Vyandarua vyenye dawa 31,916,335 (sawa na asilimia 143 ya lengo la Ilani) bila malipo kwa wananchi katika mikoa yote nchini ili kujikinga na malaria.

(viii) Kuanzishwa kwa vituo 72 vya kutoa matibabu ya Kifua Kikuu Sugu kutoka hospitali pekee ya Kibong'oto mwaka 2015 na hivyo kusogeza huduma na wananchi. Vile vile, zimenunuliwaa na kusambazwa mashine za "Gene Expert Mashine"zipatazo 209 za kutoa majibu ya ugonjwa wa kifua kikuu ndani ya masaa 2 badala ya mashine za CT Scan zinazotoa majibu baada ya masaa 48; na

(ix) Kuongeza watumishi wa afya kwa kuajiri watumishi 10,405 wa kada mbalimbali za afya kati ya mwaka 2016/17 na mwaka 2017/18. Vile vile, watumishi 612 wamegharamiwa mafunzo ndani na nje ya nchi katika ngazi ya Shahada na Uzamili.

SURA YA PILI

MAPITIO YA MWENENDO NA MWELEKEO WA UCHUMI KATIKA KIPINDI CHA MUDA WA KATI

2.1. Utangulizi

23. Katika mwaka 2018, Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) ilifanya zoezi la mapitio ya kubadilisha mwaka wa kizio kwa Pato Ghafi la Taifa kutoka mwaka 2007 na kuwa mwaka 2015. Zoezi hili linamaanisha kubadili mwaka wa kizio unaotumika katika kukusanya wastani wa bei kutoka mwaka wa zamani kuja mwaka mpya na wa hivi karibuni. Zoezi hili ni utekelezaji wa mapendekezo ya Kamisheni ya Takwimu ya Umoja wa Mataifa ambayo inashauri nchi wanachama kufanya zoezi hili kila baada ya miaka mitano.

24. Kwa ujumla, hakuna mabadiliko yenye athari kubwa kwenye muundo wa uchumi ambapo sekta za kilimo, biashara na ujenzi zinaendelea kuongoza kwenye mchango wa Pato la Taifa. Katika nusu ya kwanza ya mwaka 2018, viashiria vya mwenendo wa uchumi vinaonesha kuwa uchumi wa Taifa ni imara. Sura hii inatoa maelezo ya mwenendo wa uchumi na maoteo kwa kipindi cha muda wa kati.

2.2. Mwenendo wa Hali ya Uchumi

2.2.1. Mapitio ya Takwimu za Pato la Taifa Kufuatia Mabadiliko ya Mwaka wa Kizio kutoka 2007 kuwa 2015

25. Matokeo ya zoezi la utayarishaji wa Takwimu za Pato la Taifa kwa kuzingatia mabadiliko ya mwaka wa kizio yanaonesha kuwa, thamani ya Pato Ghafi la Taifa kwa mwaka mpya wa kizio 2015 liliongezeka kwa asilimia 6.3 na kuwa Shilingi bilioni 96,537.3 kutoka Shilingi bilioni 90,854.2 kwa mwaka wa kizio 2007. Kwa ujumla, hakuna mabadiliko yenye athari kubwa kwenye muundo wa uchumi ambapo sekta za kilimo, biashara na ujenzi zinaendelea kuongoza kwenye mchango wa Pato la Taifa.

2.2.2. Ukuaji wa Pato la Taifa

26. Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita (2013-2017), Uchumi wa Taifa umeendelea kuwa imara ambapo Pato halisi la Taifa limekua kwa wastani wa asilimia 6.9. Kwa mwaka 2017, Pato la Taifa limeendelea kukua kwa kiwango kikubwa kuliko nchi nyingine za Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa asilimia 7.1 ikilinganishwa na asilimia 7.0 kwa mwaka 2016 ikufuatiwa na Rwanda (asilimia 6.1); Kenya (asilimia 4.8); Uganda (asilimia 4.5); na Burundi (asilimia 0.0). Shughuli za kiuchumi zilizokua kwa kiasi kikubwa ni Ujenzi (asilimia 15.1); Mawasiliano

(asilimia 12.5); shughuli za utawala (asilimia 9.5); na maji (asilimia 8.5). Aidha, kasi ya ukuaji katika sekta ya kilimo ambayo ndio yenye mchango mkubwa katika Pato la Taifa, iliongezeka kutoka asilimia 5.6 kwa mwaka 2016 hadi asilimia 7.1 kwa mwaka 2017 kutokana na jitihada za Serikali kuongeza upatikanaji wa pembejeo za kilimo, zana za kilimo, ujenzi wa maghala ya kimkakati ya kuhifadhi nafaka, upanuzi wa miundombinu ya umwagiliaji pamoja na hali ya hewa nzuri.

27. Katika robo ya kwanza ya mwaka 2018, Pato halisi la Taifa limekua kwa asilimia 8.4 ikilinganishwa na asilimia 5.7 katika kipindi kama hicho mwaka 2017. Ukuaji huu umechangiwa na ongezeko la uzalishaji wa mazao na uhimilivu wa huduma za usafirishaji. Shughuli za kiuchumi ambazo zimekua kwa kiwango kikubwa ni pamoja na: ujenzi (asilimia 20); habari na mawasiliano (asilimia 18.3); utawala na ulinzi (asilimia 15.5), na shughuli za Kitaalam, Kisayansi na Kiufundi (asilimia 11.3). Aidha, shughuli za kilimo zilikua kwa asilimia 7.1.

28. Tathmini ya viashiria vya ukuaji wa uchumi vinaonyesha mwenendo mzuri katika nusu ya kwanza ya mwaka 2018 ikilinganishwa na kipindi kama hicho mwaka 2017. Viashiria hivyo ni pamoja na; mikopo kwa sekta binafsi, ujazi wa fedha; thamani ya malighafi za viwandani zilizoagizwa kutoka nje; na kodi za walaji na wazalishaji. Aidha, taarifa ya mwezi Julai 2018 ya Shirika la Fedha la Kimataifa ya Mtazamo wa Kiuchumi Duniani (World Economic Outlook) inaonesha kuwa thamani ya uzalishaji mali duniani imekua kwa asilimia 3.7 kwa mwaka 2017 na inatarajiwa kukua kwa asilimia 3.9 kwa mwaka 2018 na 2019 kwa matarajio ya kuimarika kwa uwekezaji na biashara duniani.

2.2.3. Mwenendo wa Mfumuko wa Bei

29. Mfumuko wa bei umeendelea kushuka na kuwa chini ya asilimia 5 kwa kipindi kirefu cha mwaka 2017/18. Hali hii inachagizwa na kuimarika kwa upatikanaji wa chakula katika masoko ya ndani na nchi jirani, kutengamaa kwa bei za mafuta katika soko la dunia, pamoja na utekelezaji madhubuti wa Sera za bajeti na fedha. Katika mwaka 2017/18, mfumuko wa bei ulikuwa wa wastani wa asilimia 4.3 kutoka wastani wa asilimia 5.3 kwa mwaka 2016/17. Mfumuko wa bei za chakula ulikuwa wa wastani wa asilimia 6.7 katika kipindi cha mapitio ikilinganishwa na asilimia 8.5 kipindi kama hicho mwaka 2017 (**Kielelezo Na. 2.1**). Mwezi Agosti 2018, mfumuko wa bei ulifikia kiwango cha chini cha asilimia 3.3 ambacho hakijawahi kufikiwa tangu mwaka 2015.

Kielelezo Na. 2.1: Mwenendo wa Mfumuko wa Bei



Chanzo: *Ofisi ya Taifa ya Takwimu*

2.2.4. Mfumuko wa Bei kwa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki

30. Katika kipindi cha mwaka 2017/18, mfumuko wa bei kwa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki umeendelea kubakia katika wigo wa tarakimu moja. Katika kipindi hicho, Rwanda ilikuwa na kiwango cha chini cha wastani wa asilimia 2.3 na Burundi kiwango cha juu cha wastani wa asilimia 7.1 (**Kielelezo Na. 2.2**).

Kielelezo Na. 2.2: Mfumuko wa Bei kwa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki



2.2.5. Ujazi wa Fedha na Karadha

31. Katika mwaka 2017/18, Benki Kuu iliendelea kutekeleza Sera ya Fedha ya kuongeza ukwasi kwenye uchumi (accommodative monetary policy) iliyoanza kutekelezwa katika nusu ya pili ya mwaka 2016/17. Sera hii ilitekelezwa ili kuchochea utoaji wa mikopo kwa sekta binafsi ili kusaidia kuendeleza shughuli mbalimbali za kiuchumi. Utekelezaji wa Sera ya Fedha ya kuongeza ukwasi katika kipindi hiki ulikusudia kuongeza utulivu wa riba ya siku moja baina ya mabenki (overnight interbank cash market rate) kwa kufuatilia na kudhibiti kiwango cha

amana za benki za biashara zilizopo Benki Kuu (clearing balances) ili ziendane na mahitaji ya msimu. Katika kipindi hiki, Benki Kuu ilishusha riba yake (discount rate) na kufikia asilimia 9 kutoka asilimia 12 mwezi Agosti 2017, na kuendelea kuongeza ukwasi katika uchumi kupitia nyenzo mbalimbali za kifedha ili kukidhi mahitaji ya ukwasi kwa sehemu husika ya soko la fedha. Vile vile, mwezi Agosti 2018, Benki Kuu ilishusha tena riba yake na kufikia asilimia 7.

32. Hatua zote hizi zilizochukuliwa na Benki Kuu ziliboresha hali ya ukwasi katika masoko ya fedha na kushusha riba ya siku moja baina ya mabenki (overnight interbank cash market rate), ambayo ilipungua na kufikia wastani wa asilimia 1.69 mwezi Juni 2018 ikilinganishwa na asilimia 4.08 mwezi Juni 2017. Vile vile, riba za dhamana za muda mfupi za Serikali (Treasury Bills) zilipungua hadi kufikia wastani wa asilimia 5.59 mwezi Juni 2018 kutoka wastani wa asilimia 7.64 mwezi Juni 2017 (**Kielelezo Na. 2.3**).

33. Pamoja na kwamba hatua zilizochukuliwa na Benki Kuu zilisaidia kushusha riba kwenye masoko ya fedha, riba za mikopo ya benki za biashara kwa sekta binafsi zimeendelea kuwa juu, huku riba za amana zikipungua. Viwango vikubwa vya riba za mikopo kwa sekta binafsi vilitokana na benki hizo kuweka tahadhari kubwa kwa wateja (risk premium) hali inayochangiwa zaidi na kuwepo kwa kiwango kikubwa cha mikopo chechefu. Riba za amana zilipungua na kufikia wastani wa asilimia 9.29 mwaka 2017/18 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 9.61 mwaka 2016/17. Wakati huo huo, riba za amana za kipindi cha mwaka mmoja zilipungua hadi wastani wa asilimia 10.52 ikilinganishwa na asilimia 11.66 mwaka 2016/17. Katika kipindi hicho, riba za mikopo ziliongezeka hadi kufikia wastani wa asilimia 17.83 mwaka 2017/18 ikilinganishwa na asilimia 16.61 mwaka 2016/17. Viwango vya riba ya mikopo ya mwaka mmoja ilifikia asilimia 18.48, ikilinganishwa na asilimia 15.49 mwaka 2016/17. Hali hii ilisababisha tofauti kati ya riba ya amana na mikopo ya mwaka mmoja kuongezeka hadi asilimia 7.98 mwaka 2017/18 kutoka asilimia 3.83 mwaka 2016/17. Kuongezeka kwa riba ya mikopo kulitokana na tahadhari zilizochukuliwa na benki za biashara ili kudhibiti mikopo chechefu na hivyo kuongeza gharama kwa wakopaji, hali ambayo inaweza kuathiri uwekezaji katika shughuli zinazochochea ukuaji wa uchumi.

34. Kutokana na utekelezaji wa Sera ya Fedha ya kuongeza ukwasi kwenye uchumi, ukuaji wa ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (extended broad money supply) uliongezeka hadi kufikia wastani wa asilimia 7.0 kwa mwaka 2017/18 ikilinganishwa na asilimia 4.5 mwaka 2016/17. Ukuaji huu ulichangiwa na kuongezeka kwa mikopo kwa sekta binafsi (**Kielelezo 2.3**). Hata hivyo, ukuaji huu wa ujazi wa fedha bado ulikuwa chini ya lengo la asilimia 12.

Kielelezo Na. 2.3: Mwenendo wa Ujazi wa Fedha



Chanzo*: Benki Kuu ya Tanzania*

35. Mikopo kwa sekta binafsi kwa mwaka 2017/18 iliendelea kuimarika kufuatia utekelezaji wa sera ya kuongeza ukwasi kwenye uchumi pamoja na hatua zilizochukuliwa na benki za biashara kufuatia agizo la Benki Kuu lililozitaka kupunguza mikopo chechefu. Mikopo kwa shughuli binafsi, hoteli na migahawa na ujenzi zilikua kwa kasi ikilinganishwa na mwaka uliotangulia (**Kielelezo 2.4**). Sehemu kubwa ya mikopo kwa sekta binafsi ilielekezwa katika shughuli binafsi ikifuatiwa na shughuli za biashara (**Kielelezo 2.5**).

36. Kasi ya ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi iliimarika na kufikia wastani wa asilimia 1.2 kwa mwaka 2017/18 ikilinganishwa na ukuaji wa wastani wa asilimia 7.3 kwa kipindi kama hicho mwaka 2016/17. Ingawa ukuaji huu ni mdogo ikilinganishwa na wa mwaka 2016/17, mikopo kwa sekta binafsi imeendelea kukua ambapo hadi kufikia mwezi Juni 2018 ilifikia asilimia 4.0 ikilinganishwa na asilimia 1.3 mwezi Juni 2017. Ukuaji wa mikopo ulijidhihirisha zaidi katika mikopo kwa shughuli binafsi, biashara na viwanda.

Kielelezo Na. 2.4: Wastani wa Ukuaji wa Mikopo ya Benki kwa Shughuli Kuu za Kiuchumi (Asilimia)



Chanzo: *Benki Kuu ya Tanzania*
Angalizo: **Badiliko la ukuaji wa mwaka kwa asilimia*

Kielelezo Na. 2.5: Mchanganuo wa Mikopo ya Benki katika Shughuli Kuu za Kiuchumi (Asilimia)



Chanzo: *Benki Kuu ya Tanzania*

2.2.6. Mwenendo wa Viwango vya Ubadilishaji Fedha

37. Katika kipindi cha mwaka 2017/18, thamani ya Shilingi ya Tanzania dhidi ya Dola ya Marekani iliendelea kuwa tulivu. Mwenendo huu ulichagizwa na usimamizi na utekelezaji wa Sera za Fedha na za bajeti. Wastani wa mwenendo wa ubadilishaji Shilingi dhidi ya Dola ya Marekani ulikuwa kati ya Shilingi 2,231.17 na Shilingi 2,264.97 kwa Dola moja ya Marekani, ikilinganishwa na kati ya Shilingi 2,171.0 na Shilingi 2,230.1 kwa Dola moja ya Marekani katika kipindi kama hicho kwa mwaka 2016/17. Hata hivyo, katika kipindi cha mwezi Machi 2018 hadi Mei 2018, thamani ya Shilingi dhidi ya Dola ya Marekani iliporomoka kwa kipindi kifupi kutokana na kushuka kwa msimu wa mauzo ya kibiashara pamoja na mapato ya utalii (**Kielelezo 2.6**).

Kielelezo Na. 2.6: Mwenendo wa thamani ya Shilingi (Shilingi ya Tanzania kwa Dola ya Marekani)



Chanzo: *Benki Kuu ya Tanzania*

2.2.7. Mwenendo wa Sekta ya Benki

38. Katika mwaka 2017/18, sekta ya benki imeendelea kuwa imara, salama na yenye kutengeneza faida, ikiwa na mitaji na ukwasi wa kutosha (**Jedwali Na. 2.1**). Katika kipindi hicho, uwiano wa mtaji wa msingi kwa rasilimali za benki ulifikia asilimia 18.2, ukiwa juu ya kiwango kinachohitajika kisheria cha asilimia 10.0, ingawa ilipungua kidogo ikilinganishwa na asilimia 18.3 iliyofikiwa mwaka 2016/17. Vile vile, uwiano wa rasilimali kwa amana zinazoweza kubadilishwa kwa muda mfupi kuwa fedha taslimu ulifikia asilimia 37.6, na kukidhi kiwango kinachohitajika kisheria cha asilimia 20, ingawa ni chini kidogo ya asilimia 38.1 iliyofikiwa mwezi Juni 2017.

39. Thamani ya rasilimali za benki ziliimarika kama inavyojidhihirisha katika mikopo chechefu ambayo ilipungua kufikia asilimia 10.2 kwa mwaka unaoishia Juni 2018 kutoka asilimia 10.6 mwishoni wa Juni 2017. Mwenendo huu ulichagizwa na agizo lililotolewa na Benki Kuu lililotaka benki za biashara kubuni mikakati ya kushusha uwiano wa mikopo chechefu kubaki ndani ya kiwango kisichozidi wastani wa asilimia 5.0 ikiwamo kuboresha utoaji, usimamizi na ulipaji mikopo, na kutumia kwa lazima taarifa ya historia za wakopaji kabla ya kutoa mkopo (mandatory use of credit reference bureau reports).

40. Katika mwezi Januari 2018, Benki Kuu ilisitisha leseni za benki za biashara zilizokuwa na mitaji pungufu chini ya kiwango kilichowekwa kisheria baada ya kushindwa kutimiza matakwa hayo ndani ya muda wa miaka mitano. Benki hizo ni Covenant Bank for Women (Tanzania) Limited, Efatha Bank Limited, Njombe Community Bank Limited, Kagera Farmers' Cooperative Bank Limited na Meru

Community Bank Limited. Vile vile, mwezi Mei 2018, Benki ya Twiga Bancorp Ltd ilikamilisha taratibu za kuunganishwa na Benki ya TPB ili kutatua tatizo la kutokuwa na mtaji wa kutosha.

Jedwali Na. 2.1: Mwenendo wa Viashiria vya Sekta ya Benki (Asilimia)

Kiashiria	Ukomo	Jun-17	Sep-17	Des-17	Mar-18	Jun-18
Utoshelevu wa mtaji						
Uwiano wa mtaji wa msingi kwa rasilimali za benki	Kiwango cha chini 10	18.3	18.9	18.9	18.7	18.2
Ukwasi						
Uwiano wa rasilimali zenye ukwasi kwa amana zinazoweza kuhitajika muda mfupi	Kiwango cha chini 20	38.1	37.9	40.3	39.1	37.6
Uwiano wa mikopo kwa amana za wateja		83.1	84.9	81.6	81.0	83.9
Mapato na faida						
Faida kutokana na uwekezaji wa rasilimali		2.3	2.0	1.6	17.0	1.6
Faida kutokana na uwekezaji wa mtaji		10.4	8.7	6.9	7.2	6.7
Ubora wa rasilimali						
Uwiano wa mikopo chechefu kwa mikopo yote		10.6	12.5	11.7	11.3	10.2

Chanzo*: Benki Kuu ya Tanzania*

2.2.8. Deni la Taifa

41. Hadi kufikia Juni, 2018 Deni la Taifa lilifikia Dola za Marekani milioni 27,774.86 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 25,350.76 kwa kipindi kama hicho mwaka 2017, ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia 9.6. Kati ya Deni hilo, Dola za Marekani milioni 23,234.26 ni deni la Serikali na Dola za Marekani million 4,540.60 ni deni la nje la sekta binafsi. Ongezeko la deni la Serikali lilitokana na kupokelewa kwa fedha za mikopo ili kugharamia miradi ya maendeleo pamoja na mikopo kwenye soko la Dhamana za Serikali kwa ajili ya kugharamia nakisi ya Bajeti.

(a) Uhimilivu wa Deni la Taifa

42. Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada SURA 134, inaitaka Serikali kufanya uchambuzi wa uhimilivu wa deni kila mwaka ambao pamoja na mambo mengine unaonyesha mwenendo wa viashiria mbalimbali vya uhimilivu wa deni ikiwa ni pamoja na maelezo ya hali halisi ya uchumi katika mitizamo mbalimbali, na kushauri hatua za kuimarisha uhimilivu wa deni. Matokeo ya hivi karibuni ya uhimilivu wa Deni la Taifa lililofanyika Novemba 2017 kwa kutumia Pato la Taifa kwa kizio cha mwaka 2007, yanaonesha kuwa deni la Taifa lipo chini ya ukomo wa hatari na ni himilivu kwa kipindi cha muda mfupi, wa kati na mrefu. Viashiria vyote vya athari za madeni vimeendelea kuwa katika wigo unaokubalika kimataifa kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 2.2**.

Jedwali Na. 2.2: Viashiria vya Uhimilivu wa Deni la Taifa

Viashiria Deni la Nje	Ukomo	2017/18	2018/19	2019/20	2027/28	2028/29	2036/37	2037/38
Deni la Nje (PV)/Pato la Taifa	40	19.7	19.8	19	12.6	12.5	12.7	12.8
Deni la Nje (PV)/Uuzaji wa Bidhaa Nje	150	81.8	83.2	80.7	56.7	56.3	57.4	57.8
Deni la Nje (PV)/Mapato ya Ndani	250	117.1	117.3	110.1	67.3	66.7	64.5	64.7
Ulipaji wa Deni Nje/Uuzaji wa Bidhaa Nje	20	9.3	8.2	10.1	6.5	6.4	5.9	6
Ulipaji wa Deni Nje/Mapato ya Ndani	20	13.3	11.6	13.8	7.7	7.5	6.6	6.7
Viashiria Deni la Nje na la Ndani								
Deni/Pato la Taifa	56	34.4	33	31.2	20.5	20.2	19.7	19
Deni/Mapato ya Ndani		194.5	183.9	170.7	107.8	105.9	99.2	95
Ulipaji wa Deni/Mapato ya Ndani		26.3	23	25.2	13.8	13.6	11.7	11.3

Chanzo: *Wizara ya Fedha na Mipango*
Angalizo: *Takwimu hizi ni kwa mujibu wa mwaka wa kizio wa 2007*

2.2.9. Mwenendo wa Sekta ya Nje

43. Katika kipindi hicho, nakisi ya Urari wa Malipo ya Kawaida iliongezeka kwa asilimia 23.7 na kufikia Dola za Marekani milioni 1,778.0 ikilinganishwa na Dola za Marekani milioni 1,437.8 kwa mwaka 2016/17. Ongezeko hili linatokana na kuongezeka kwa thamani ya bidhaa zilizoagizwa kutoka nje ya nchi pamoja na malipo ya riba za mikopo nje ya nchi.

44. Akiba ya fedha za kigeni ilikuwa Dola za Marekani milioni 5,483.9 mwishoni mwa mwezi Juni 2018 ikilinganishwa na Dola za Marekani milioni 5,000.4 mwishoni mwa mwezi Juni 2017, ambayo inatosheleza kuagiza bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa kipindi cha takriban miezi 5.6.

45. Mwaka 2017/18, thamani ya mauzo ya bidhaa na huduma nje iliongezeka kwa asilimia 2.8 ikilinganishwa na mwaka 2016/17. Ongezeko hili lilichangiwa na kuongezeka kwa thamani ya mauzo ya korosho, karafuu, tumbaku, chai na katani ambapo mauzo hayo yaliongezeka kwa asilimia 33.0. Vile vile, mafanikio haya yalitokana na hali nzuri ya hewa pamoja na jitihada za Serikali katika kuendeleza kilimo ikiwamo ugawaji bure wa baadhi ya vifaa vya kilimo, pamoja na kuimarika kwa bei za bidhaa katika soko la dunia. Hata hivyo, thamani ya mauzo ya kahawa na pamba nje yalipungua kutokana na uchache wa mauzo (**Jedwali 2.3**).

46. Katika kipindi cha mapitio, mauzo ya bidhaa za viwandani na dhahabu nje ya nchi yaliongezeka sambamba na kuimarika kwa bei za bidhaa kwenye soko la dunia. Mauzo ya bidhaa za viwandani yaliongezeka kwa asilimia 8.2 na kufikia dola za Marekani milioni 833.8 kutoka dola za Marekani milioni 770.5 mwaka 2016/17 ikichagizwa na ongezeko la mauzo ya sabuni, bidhaa za plastiki na makaratasi nje.

47. Thamani ya uagizaji wa bidhaa na huduma nje iliongezeka kwa asilimia 4.7 kutoka Dola za Marekani milioni 9,701.1 mwaka 2016/17. Ongezeko hili lilitokana na kuongezeka kwa uagizaji wa bidhaa za walaji kwa asilimia 5.7 ikifuatiwa na bidhaa za kati na malighafi za viwandani.

Jedwali Na. 2.3: Urari wa Malipo ya Kawaida

Dola za Marekani Milioni

	2016/17	2017/18[P]	Badiliko %
Bidhaa	**-2,774.7**	**-2,860.3**	**3.1**
Mauzo Nje	4,932.4	5,093.8	3.3
Uagizaji Nje	7,707.2	7,954.0	3.2
Huduma	**1,775.3**	**1,652.1**	**-6.9**
Mapato	3,769.2	3,855.7	2.3
Malipo	1,994.0	2,203.6	10.5
Bidhaa na Huduma	**-999.5**	**-1,208.2**	**20.9**
Mauzo ya bidhaa na huduma	8,701.7	8,949.4	2.8
Uagizaji bidhaa na huduma	9,701.1	10,157.6	4.7
Mapato ya Vitega uchumi	**-893.7**	**-1,004.2**	**12.4**
Mapato	105.6	138.6	31.3
Malipo	999.3	1,142.8	14.4
Uhamisho wa Mali	**455.5**	**434.4**	**-4.6**
Zilizoingia	520.4	521.1	0.1
Kwa Serikali Kuu	157.9	155.3	-1.6
Zilizotoka	65.0	86.6	33.4
Urari wa Malipo ya Kawaida	**-1,437.7**	**-1,778.0**	**23.7**

Chanzo: *Benki Kuu ya Tanzania*

2.3. Mwelekeo wa Uchumi Jumla na Maoteo ya Muda wa Kati

48. Ili kufikia malengo ya Serikali, baadhi ya misingi iliyozingatiwa katika kuweka malengo ya uchumi jumla na kisera katika kipindi cha muda wa kati (2019/20 - 2021/22) ni pamoja na: kuendelea kuimarishwa na kudumishwa kwa amani, usalama, utulivu na umoja wa ndani na nchi jirani; kuimarika kwa viashiria vya uchumi jumla na maendeleo ya kiuchumi na kijamii kama vile Pato la Taifa, ukusanyaji wa mapato ya ndani na mfumuko wa bei; kuendelea kuimarika na kutengamaa kwa uchumi wa dunia; kuendelea kuwa na utulivu wa bei za mafuta katika soko la dunia; na hali nzuri ya hewa ndani ya nchi na katika nchi jirani.

2.3.1. Mwelekeo wa Ukuaji wa Uchumi Duniani

49. Kwa mujibu wa Taarifa ya Mwelekeo wa Uchumi wa Dunia ya Julai 2018,

Nchi Zinazoendelea na Kuibukia Kiuchumi zinatarajiwa kukua kwa asilimia 4.9 mwaka 2018 ikilinganishwa na asilimia 4.7 mwaka 2017 na kuendelea kuimarika kufikia asilimia 5.1 kwa mwaka 2019. Uchumi wa China unatarajiwa kupungua kidogo kutoka asilimia 6.9 mwaka 2017 na kufikia asilimia 6.6 kwa mwaka 2018 wakati uchumi wa India unatarajiwa kukua kwa asilimia 7.3 mwaka 2018 kutoka asilimia 6.7 mwaka 2017.

50. Katika nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara, uchumi unatarajiwa kukua kwa asilimia 3.4 mwaka 2018 ikilinganishwa na kiwango cha ukuaji cha asilimia 2.8 mwaka 2017. Uchumi wa nchi hizo unatarajiwa kuendelea kuimarika kufikia ukuaji wa asilimia 3.9 mwaka 2019. Kati ya Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, Tanzania na Rwanda zinatarajiwa kuwa na viwango vya juu vya ukuaji wa asilimia 7.2 mwaka 2018, zikifuatiwa na Kenya (asilimia 5.5); Uganda (asilimia 5.2); na Burundi kuendelea kuimarika na kukua kwa asilimia 0.4 ifikapo mwaka 2019 (**Jedwali Na. 2.4**).

Jedwali Na. 2.4: Ukuaji wa Uchumi wa Dunia na Maoteo (Asilimia)

	Halisi			Maoteo	
	2015	**2016**	**2017**	**2018**	**2019**
Dunia	3.1	3.2	3.7	3.9	3.9
Nchi zilizoendelea	2.1	1.7	2.4	2.4	2.2
Nchi zinazoendelea na Kuibukia	4.3	4.3	4.7	4.9	5.1
Nchi zinazoendelea za Asia	6.8	6.4	6.5	6.5	6.5
China	6.9	6.7	6.9	6.6	6.4
India	8.0	7.1	6.7	7.3	7.5
Nchi za Afrika, Kusini mwa Jangwa la Sahara	3.4	1.3	2.8	3.4	3.8
Tanzania	7.0	7.0	7.1	7.2	7.3
Kenya	5.6	6.0	4.8	5.5	6.0
Uganda	4.8	4.9	4.5	5.2	5.8
Rwanda	6.9	6.0	6.1	7.2	7.8
Burundi	-4.0	-0.5	0.0	0.1	0.4

Chanzo: *Shirika la Fedha la Kimataifa, Julai, 2018*

2.3.2. Maoteo ya Ukuaji wa Pato la Taifa katika Kipindi cha Muda wa Kati

51. Inatarajiwa kwamba uzingatiaji wa misingi ya utekelezaji mzuri wa Sera za Serikali ikijumuisha utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, utaimarisha kasi ya ukuaji wa Pato la Taifa kufikia asilimia 7.2 kwa mwaka 2018 na kufikia wastani wa asilimia 7.6 katika kipindi cha muda wa kati (**Kielelezo Na. 2.8**). Mwenendo wa ukuaji katika kipindi cha muda wa kati unachagizwa na jitihada za Serikali kuendeleza ufuaji wa umeme hususan kwa kutumia nguvu ya maji; kuimarika kwa huduma za usafirishaji; uwekezaji katika sekta ya majengo ya biashara; uendelezaji wa ujenzi wa miradi ya miundombinu; na azma ya Serikali ya kujenga uchumi wa viwanda.

2.3.3. Maoteo ya Ukuaji Kisekta

52. **Shughuli za Ujenzi** zinatarajiwa kukua kwa wastani wa asilimia 15.1 kwa mwaka 2018 na kukua kwa wastani wa asilimia 14.4 katika kipindi cha muda wa kati, kutokana na kuendelea na utekelezaji wa miradi mikubwa ya miundombinu ikiwa ni pamoja na ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha *standard gauge*; Ubungo *Interchange;* kuimarisha mtandao wa barabara na madaraja; ukamilishaji wa jengo la III la abiria katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere; na upanuzi wa viwanja vingine vya ndege nchini.

53. **Shughuli za Uzalishaji Viwandani** zinatarajiwa kukua kwa asilimia 8.0 kwa mwaka 2018 na kwa wastani wa asilimia 7.8 katika kipindi cha muda wa kati, ikichangiwa na matarajio ya uzalishaji kutoka miradi mbalimbali kama ya umeme vijijini na mijini, pamoja na jitihada za Serikali kukuza viwanda kupitia uboreshaji wa mazingira wezeshi kwa uendeshaji wa biashara na uwekezaji ili kuvutia sekta binafsi kushiriki katika kukuza viwanda. Matarajio ni kuongezeka kwa uzalishaji katika kipindi cha muda mrefu baada ya kukamilika kwa ujenzi wa miundombinu wezeshi na ujenzi wa viwanda unaoendelea.

54. **Uchimbaji Madini** unatarajiwa kukua kwa asilimia 4.0 katika mwaka 2018 na kuongezeka kufikia wastani wa asilimia 4.1 katika kipindi cha muda wa kati kutokana na matarajio ya kuimarika kwa udhibiti na usimamizi wa madini pamoja na kuimarika kwa bei ya dhahabu duniani ambayo itaongeza shughuli za uchimbaji.

55. **Uzalishaji Umeme na Gesi** unatarajiwa kuongezeka kwa asilimia 2.9 mwaka 2018 na kukua kwa wastani wa asilimia 3.0 katika kipindi cha muda wa kati. Ukuaji huu unachagizwa na matarajio ya ongezeko la uzalishaji umeme kutoka vyanzo mbalimbali kama gesi asilia, maji, mvuke, upepo na makaa ya mawe pamoja na kuimarika kwa usambazaji kwenye gridi ya taifa. Katika kipindi hiki, miradi mikubwa inayotarajiwa kutekelezwa ni mradi wa ufuaji wa umeme wa maji Mto Rufiji (Megawati 2,100) na utekelezaji wa Mpango Kabambe wa Umeme Vijijini kupitia Mradi Kabambe wa Kusambaza Umeme Vijijini Awamu ya Tatu (REA III) ambao ni sehemu ya Mpango Kabambe wa Sekta ya Umeme.

56. **Shughuli za Usafirishaji** zinatarajiwa kukua kwa asilimia 6.9 kwa mwaka 2018 na kufikia wastani wa asilimia 7.1 katika kipindi cha muda wa kati. Ukuaji huu unachagizwa na matarajio ya kuongezeka kwa usafirishaji wa mizigo na abiria kwa njia ya reli, barabara na anga; kuongeza uwezo na ufanisi wa Bandari za Dar es Salaam, Mtwara na Tanga; na kuongezeka kwa usafirishaji wa gesi asilia kupitia bomba la gesi kutoka Mtwara na Lindi hadi Dar es Salaam.

57. **Huduma za Malazi na Migahawa** zinatarajiwa kukua kwa kiwango cha asilimia 2.4 kwa mwaka 2018 na kufikia ukuaji wa wastani wa asilimia 2.8 katika kipindi cha muda wa kati. Hali hii inachagizwa na ukuaji mkubwa wa shughuli za kitalii zinazothibitishwa na ongezeko la idadi ya wageni kutoka nje na bidhaa mseto (ukanda wa kitalii kusini mwa Tanzania; utambuzi wa maeneo mapya ya utalii; utalii wa urithi); na kuhamasisha utalii wa ndani na jitihada za Serikali kuboresha miundombinu wezeshi ya kitalii.

58. **Shughuli za Utawala** zinatarajiwa kukua kwa kiwango cha asilimia 9.5 kwa mwaka 2018 na kuendelea kufikia wastani wa asilimia 9.6 katika kipindi cha muda wa kati kutokana na matarajio ya kuongezeka kwa matumizi kwenye maboresho katika sekta ya umma (maboresho ya Utumishi wa Umma, Serikali za Mitaa, Sheria, Usimamizi wa Fedha za Umma, mazingira ya Biashara na Uwekezaji, na Mkakati na Mpango wa Taifa wa Kupambana na Rushwa), ajira mpya kuziba pengo lililopo; matumizi ya Serikali katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa mwaka 2019 na Uchaguzi Mkuu mwaka 2020.

Kielelezo Na. 2.8: Ukuaji Halisi na Maoteo ya Pato la Taifa



Chanzo: *Wizara ya Fedha na Mipango*

2.3.4. Mfumuko wa Bei Katika Kipindi cha Muda wa Kati

59. Mfumuko wa bei unatarajiwa kufikia asilimia 4.8 ifikapo Desemba 2018 kufuatia ongezeko la bei ya mafuta katika soko la dunia kutokana na matarajio ya kupungua kwa uwezo wa uzalishaji nchini Venezuela pamoja na vikwazo vya kiuchumi vya Marekani dhidi ya Iran ambavyo vitasababisha ugumu wa ongezeko la uzalishaji wa mafuta kwa nchi zinazozalisha mafuta kwa wingi (*OPEC)* na nchi

zisizo za *OPEC*. Mfumuko wa bei unatarajiwa kufikia asilimia 5.0 mpaka Juni 2019 na kuendelea kubaki katika wastani huo katika kipindi cha muda wa kati kutokana na sababu zifuatazo: kupungua kwa gharama za uzalishaji kutokana na kuimarika kwa uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa umeme wa uhakika na nafuu; kuimarika kwa bei ya mafuta katika soko la dunia; Sera imara za fedha na bajeti; na hali ya hewa nzuri nchini.

2.3.5. Sera ya Fedha

60. Katika mwaka 2018/19, Benki Kuu inategemea kuanza kutekeleza Mfumo wa Sera ya Fedha unaozingatia Riba ya Benki Kuu (*Central Bank Rate - CBR*), ili kuongeza ufanisi wa sera ya fedha katika kufikia malengo ya utulivu wa bei na ukuaji wa uchumi. Chini ya mfumo huu, Benki Kuu itatumia mwenendo wa riba za muda mfupi (*interbank cash market interest rate*) kama kiashiria cha msingi cha hali ya ukwasi badala ya ujazi wa fedha taslimu (*reserve money*).

61. Ujazi wa Fedha kwa Tafsiri Pana Zaidi (M3) unatarajiwa kuendelea kukua sanjari na ukuaji wa shughuli mbalimbali za kiuchumi na kuimarika kwa mzunguko wa fedha. Ukuaji wa M3 unatarajia kuimarika kufikia asilimia 12.2 Juni 2019 kutoka ukuaji wa asilimia 6.0 ulioshuhudiwa Juni 2018, wakati huo mikopo ya benki kwa sekta binafsi inakadiriwa kukua kwa wastani wa asilimia 10.2 kutoka asilimia 4.0. Katika kipindi cha muda wa kati, ukuaji wa M3 unatarajiwa kuwa katika kiwango cha asilimia 11.5, wakati mikopo ya benki kwa sekta binafsi itakua kwa wastani wa asilimia 9.0.

2.3.6. Sekta ya Nje

62. Urari wa malipo ya kawaida unatarajiwa kuwa na nakisi ya asilimia 4.3 ya Pato la Taifa kwa mwaka 2018/19 ikilinganishwa na nakisi ya asilimia 3.3 katika mwaka uliotangulia. Katika kipindi cha muda wa kati, urari wa malipo ya kawaida unatarajiwa kuwa na nakisi ya wastani wa asilimia 4.5 ya Pato la Taifa kutokana na ongezeko kubwa la uagizaji wa bidhaa za mtaji kwa ajili ya ujenzi wa miradi mikubwa ya miundombinu ikilinganishwa na mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi.

63. Mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi kwa mwaka 2018/19 yanatarajiwa kufikia asilimia 16.3 ya Pato la Taifa, ikilinganishwa na asilimia 16.7 kwa mwaka 2017/18. Katika kipindi cha muda wa kati, mauzo ya bidhaa na huduma nje yanatarajiwa kufikia wastani wa asilimia 12.1 ya Pato la Taifa.

64. Uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi unakadiriwa kufikia asilimia 19.6 ya Pato la Taifa mwaka 2018/19 ikilinganishwa na asilimia 18.9 kwa

mwaka uliotangulia. Ongezeko hili la uagizaji wa bidhaa na huduma nje ya nchi ni kutokana na kuimarika kwa shughuli za kiuchumi kama vile utekelezaji wa miradi mikubwa ya uwekezaji ikijumuisha ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha *standard gauge*, mradi wa kuzalisha umeme wa maji katika mto Rufiji na ujenzi wa bomba la mafuta ghafi kutoka Hoima (Uganda) hadi Tanga. Katika kipindi cha muda wa kati uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi unatarajiwa kuwa wa wastani wa asilimia 19.8 ya Pato la Taifa.

SURA YA TATU

MPANGO NA BAJETI KWA MUDA WA KATI

3.1. Utangulizi

65. Jukumu la msingi la Serikali, katika mpango na bajeti, ni kutunga na kutekeleza sera wezeshi za kibajeti ili kuchochea uwekezaji, ukuaji wa uchumi na kuboresha ustawi wa watu. Ili kufikia malengo ya muda wa kati, sera mahususi za kibajeti zitaandaliwa ili kufanikisha utekelezaji wa ajenda ya Taifa ya Maendeleo ya Viwanda na Watu. Serikali itaelekeza rasilimali fedha kwenye miradi ya kipaumbele yenye matokeo makubwa kiuchumi na kuongeza mapato ya Serikali. Vile vile, matumizi ya mifumo ya kisasa ya TEHAMA na hatua madhubuti za kiutawala zitawezesha kuleta ufanisi katika ukusanyaji, utengaji na usimamizi wa mapato.

3.2. Sera za Mapato na Makadirio

3.2.1. Sera za Mapato ya Ndani

66. Katika kipindi cha muda wa kati, lengo la sera ya mapato ya ndani ni kuimarisha makusanyo kwa kuendelea;

(i) Kuboresha mazingira ya kufanya biashara ili kuvutia uwekezaji, ukuaji wa biashara ndogondogo na za kati pamoja na ukuaji wa uchumi endelevu;

(ii) Kuboresha mazingira ya ulipaji kodi kwa hiari, upanuzi wa wigo wa kodi na matumizi ya mifumo ya TEHAMA katika usimamizi wa kodi;

(iii) Kuimarisha usimamizi wa sheria za kodi ili kutatua changamoto za ukwepaji kodi na kupunguza upotevu wa mapato;

(iv) Kuimarisha makusanyo yasiyo ya kodi kwa kuhimiza matumizi sahihi ya mifumo ya TEHAMA katika ukusanyaji wa mapato;

(v) Kuwianisha na kupunguza tozo na ada mbalimbali zinazotozwa na Wakala za Serikali na Mamlaka za Udhibiti; na

(vi) Kuwajengea uwezo maafisa wa Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala na Halmashauri ili kuimarisha uwezo wa ukusanyaji wa mapato yasiyo ya kodi.

3.2.2. Makadirio ya Mapato ya Ndani

67. Mapato ya ndani (yakijumuisha mapato ya Halmashauri) yanakadiriwa kuongezeka hadi Shilingi bilioni 23,206.8 mwaka 2019/20 kutoka Shilingi bilioni 20,894.6 mwaka 2018/19 na unakadiriwa kuongezeka kwa wastani wa asilimia 10.1 katika kipindi cha muda wa kati hadi Shilingi bilioni 28,113.9 mwaka 2021/22. Mapato ya ndani katika Pato la Taifa yanakadiriwa kuongezeka kutoka asilimia 14.6 mwaka 2019/20 hadi asilimia 14.9 mwaka 2021/22. Vile vile, mapato ya ndani katika bajeti yanakadiriwa kuongezeka kutoka asilimia 69.3 mwaka 2019/20 hadi asilimia

73.6 mwaka 2021/22.

68. Mapato ya kodi yanakadiriwa kuongezeka kwa asilimia 11.8 hadi Shilingi bilioni 20,124.1 mwaka 2019/20 kutoka Shilingi bilioni 18,000.2 mwaka 2018/19 na kukua kwa wastani wa asilimia 10.1 katika kipindi cha muda wa kati hadi Shilingi bilioni 24,385.4 mwaka 2021/22. Mapato ya kodi katika Pato la Taifa yanakadiriwa kuongezeka kutoka asilimia 12.7 mwaka 2019/20 hadi asilimia 12.9 mwaka 2021/22.

69. Mapato Yasiyo ya Kodi (yakijumuisha mapato ya Halmashauri) yanakadiriwa kuongezeka hadi Shilingi bilioni 3,082.7 mwaka 2019/20 kutoka Shilingi bilioni 2,894.4 mwaka 2018/19. Aidha, mapato yasiyo ya kodi yanakadiriwa kukua kwa wastani wa asilimia 10.0 na kufikia Shilingi bilioni 3,728.5 mwaka 2021/22 ambapo mapato hayo yanakadiriwa kuwa asilimia 2.0 ya Pato la Taifa katika kipindi cha muda wa kati.

Kielelezo Na. 3.1: Makadirio ya Mapato Kwa Kipindi cha Muda wa Kati (*Shilingi Bilioni)*



Chanzo: Wizara ya Fedha na Mipango

70. Ili kufikia malengo ya makadirio ya mapato ya ndani, Serikali imeandaa mikakati mahsusi ya kiutawala itakayotekelezwa katika kipindi cha muda wa kati. Mikakati hiyo inajumuisha:

(i) Kutekeleza Mfumo Jumuishi wa Usimamizi wa Mapato ya Ndani (IDRAS) ili kuongeza ufanisi katika usimamizi wa makusanyo ya kodi za ndani;

(ii) Kupanua wigo wa kodi kupitia utambuzi na usajili wa walipakodi wapya, kuwafikia walipa kodi wasiolipa kodi kwa hiari, pamoja na kuendelea na zoezi la urasimishaji wa sekta isiyo rasmi;

(iii) Kuboresha utendaji wa Mfumo wa Usimamizi wa Mashine za Risiti za Kieletroniki (EFDMS) ili kuimarisha usimamizi wa matumizi ya Mashine za Risiti za Kielektroniki (EFD);

(iv) Kuimarisha uwezo wa ufuatiliaji na udhibiti wa uhamishaji haramu wa fedha unaofanywa na kampuni za kimataifa kwa kuanzisha Kanzidata ya Ubadilishanaji Taarifa (EOI);

(v) Kuimarisha viwango vya huduma kwa Mlipakodi kwa kuanzisha vituo vya ushauri katika maeneo yenye mzunguko mkubwa wa biashara;

(vi) Kuimarisha usimamizi wa misamaha ya kodi;

(vii) Kuimarisha Mfumo wa Serikali wa Kielektroniki wa Ukusanyaji wa Mapato (GePG) ili kuongeza ufanisi katika ukusanyaji wa mapato; na

(viii) Kuimarisha mifumo ya ufuatiliaji katika taasisi za Serikali ili kuhakikisha kuwa michango stahiki ya Mashirika kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali inawasilishwa kwa wakati.

Kielelezo Na. 3.2: Mchanganuo wa Mapato Katika Kipindi cha Muda wa Kati (2019/20 – 2021/22) ***Shilingi Bilioni***



Chanzo: Wizara ya Fedha na Mipango

3.3. Sera za Matumizi na Makadirio

3.3.1. Sera za Matumizi

71. Sera za Matumizi katika kipindi cha muda wa kati zitajumuisha yafuatayo: -

(i) Kusimamia nidhamu ya matumizi ya fedha za umma na kuendelea kupunguza matumizi yasiyo ya lazima;

(ii) Kuelekeza fedha kwenye maeneo ya kipaumbele ili kuchochea ukuaji wa uchumi;

(iii) Kudhibiti ulimbikizaji wa madeni; na

(iv) Kuhakikisha kuwa nakisi ya bajeti haizidi asilimia 3.0 ya Pato la Taifa.

3.3.2. Makadirio ya Matumizi

72. Matumizi ya Serikali yanakadiriwa kukua hadi Shilingi bilioni 33,500.2 mwaka 2019/20 (sawa na asilimia 21.1 ya Pato la Taifa) kutoka Shilingi bilioni 32,476.0 mwaka 2018/19. Vile vile, matumizi yanakadiriwa kukua kwa wastani wa asilimia 6.7 hadi Shilingi bilioni 38,172.5 mwaka 2021/22 (sawa na asilimia 20.2 ya Pato la Taifa).

Kielelezo Na 3.3: Mwenendo wa Makadirio ya Matumizi katika Kipindi cha Muda wa Kati (2019/20 – 2021/22) (Shilingi bilioni)



Chanzo: Wizara ya Fedha na Mipango

73. Matumizi ya Kawaida yanakadiriwa kuongezeka kwa asilimia 3.2 hadi Shilingi bilioni 21,115.8 mwaka 2019/20 (sawa na asilimia 13.3 ya Pato la Taifa) na kukua kwa wastani wa asilimia 8.0 hadi Shilingi bilioni 24,612.6 mwaka 2021/22 (sawa na asilimia 13.0 ya Pato la Taifa). Matumizi ya Maendeleo yanakadiriwa kuwa Shilingi bilioni 12,384.4 mwaka 2019/20 na kuongezeka hadi Shilingi bilioni 13,559.8 mwaka 2021/22.

Kielelezo Na. 3.4: Makadirio ya Matumizi katika Kipindi cha Muda wa Kati kwa Aina Kuu ya Matumizi (Shilingi bilioni)



Chanzo: Wizara ya Fedha na Mipango

3.3.3. Uainishaji wa Makadirio ya Matumizi Kiuchumi (2019/20 – 2021/22)

74. Katika mwaka 2019/20, mishahara (ikijumuisha mishahara ya Taasisi) inakadiriwa kuwa Shilingi bilioni 7,559.0 (sawa na asilimia 33.7 ya makadirio ya mapato ya ndani ya Serikali Kuu) na kukadiriwa kuongezeka hadi Shilingi bilioni 8,422.7 mwaka 2021/22 (sawa na asilimia 31.0 ya makadirio ya mapato ya ndani ya Serikali Kuu). Malipo ya mtaji kwa deni la ndani na nje yanakadiriwa kupungua kutoka Shilingi bilioni 6,269.7 mwaka 2018/19 hadi Shilingi bilioni 6,006.4 mwaka 2019/20 (sawa na asilimia 3.8 ya Pato la Taifa) na kukadiriwa kuongezeka hadi Shilingi bilioni 7,895.0 (sawa na asilimia 4.2 ya Pato la Taifa) mwaka 2021/22.

75. Katika mwaka 2019/20, malipo ya riba yanakadiriwa kuongezeka hadi Shilingi bilioni 2,619.2 na kuendelea kuongezeka hadi Shilingi bilioni 3,128.7 mwaka 2021/22. Malipo ya riba yanakadiriwa kuwa asilimia 1.7 ya Pato la Taifa katika kipindi chote cha muda wa kati.

76. Kiasi cha kulipia bidhaa, huduma na ruzuku kinakadiriwa kuwa Shilingi bilioni 4,931.2 mwaka 2019/20 sawa na asilimia 3.1 ya Pato la Taifa na kuongezeka hadi Shilingi bilioni 5,166.1 sawa na asilimia 2.7 ya Pato la Taifa mwaka 2021/22.

Kielelezo Na. 3.5: Uainishaji wa Makadirio ya Matumizi Kiuchumi (2019/20 – 2021/22) (Shilingi milioni)



Chanzo: Wizara ya Fedha na Mipango

77. Matumizi makubwa ya Serikali katika kipindi cha muda wa kati yataelekezwa katika miradi ya kimkakati inayoendelea ikiwa ni pamoja na ujenzi wa Reli Mpya ya Kati kwa kiwango cha *Standard Gauge* (SGR); ujenzi wa Mtambo wa Kufua Umeme wa Maji Rufiji; Kuboresha Shirika la Ndege (ATCL); uendeshaji wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere Terminal III; usambazaji wa umeme vijijini; miundombinu ya umwagiliaji; upanuzi wa Bandari ya Dar es Salaam, Mtwara na Tanga; na ujenzi wa Vivuko vipya na Meli kwenye Maziwa Makuu. Matumizi mengine ni pamoja na kulipa deni la Taifa; ulipaji wa mishahara; utekelezaji wa miradi yenye kuongeza mapato katika Mamlaka za Serikali za Mitaa; utoaji wa elimumsingi bila ada; Uchaguzi wa Serikali za Mitaa; maandalizi ya Uchaguzi Mkuu; ujenzi wa barabara za juu Ubungo; Utoaji wa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu; na utoaji wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi.

3.3.4. Uainishaji wa Makadirio ya Matumizi Kulingana na Majukumu ya Serikali (CoFoG) (2019/20 – 2021/22)

78. CoFoG inaainisha utoaji wa fedha za Serikali kwa kuzingatia majukumu kama vile afya; elimu; ulinzi na utawala[1]. Katika kipindi cha muda wa kati, sehemu kubwa ya mgawanyo wa matumizi kwa kuzingatia majukumu itaelekezwa kwenye shughuli za kutoa huduma za mihimili ya utawala ambazo zinajumuisha ulipaji wa deni la Taifa, ikifuatiwa na masuala ya uchumi, elimu, ulinzi na afya kama inavyoonekana kwenye **Kielelezo Na. 3.6**. Makadirio ya matumizi ya kina kwa makundi yameoneshwa kwenye **Kiambatisho Na. 1**.

Kielelezo Na. 3.6: Uainishaji wa Makadirio ya Matumizi kwa Majukumu (Shilingi milioni)



Chanzo: Wizara ya Fedha na Mipango

3.3.5. Misaada na Mikopo

79. Katika kipindi cha muda wa kati, Serikali itahakikisha inakidhi mahitaji ya nakisi ya bajeti kwa gharama ya chini inayoendana na uangalifu wa vihatarishi pamoja na kusaidia kukuza maendeleo ya soko la fedha la ndani. Vile vile, uhamasishaji wa misaada kwa ajli ya bajeti ya Serikali utazingatia miadi ya Washirika wa Maendeleo katika kipindi cha muda wa kati.

(a) Misaada

80. Katika kipindi cha muda wa kati, Serikali itaendelea kuimarisha ushirikiano

[1] Kwa mujibu wa Umoja wa Mataifa

wa kimaendeleo na Washirika wa Maendeleo ili kuhakikisha wanatimiza ahadi zao kama ilivyopangwa. Ili kuimarisha upatikanaji wa fedha za Washirika wa Maendeleo, na kufanya ushirikiano wa maendeleo kuwa madhubuti, Serikali itatekeleza Mpango kazi wa Kutekeleza Mwongozo wa Ushirikiano wa Kimaendeleo. Mpango kazi utatekelezwa katika ngazi zote za Serikali kupitia mifumo ya kitaifa iliyopo, kisekta na ngazi za chini kwa nyanja zote za mahusiano na Washirika wa Maendeleo. Kupitia utekelezaji wa Mpango Kazi, Serikali itaendelea kujumuisha na kuratibu jitihada za wadau wote wa maendeleo ambao ni muhimu katika kuongeza ufanisi katika ushirikiano wa kimaendeleo.

81. Katika kipindi cha muda wa kati, misaada kutoka kwa Washirika wa Maendeleo inatarajiwa kuongezeka kutoka Shilingi bilioni 1,343.3 mwaka 2019/20 hadi Shilingi bilioni 1,380.7 mwaka 2021/22. Misaada ya Kibajeti inatarajiwa kupungua baada ya mwaka 2019/20, kipindi ambacho programu ya Misaada ya Kibajeti kutoka Jumuiya ya Ulaya itafikia ukomo. Hata hivyo, upungufu huo utafidiwa na fursa ya nyongeza ya Misaada ya Kibajeti kutoka nchi washirika. Kwa upande mwingine, michango katika mifuko ya pamoja ya kisekta na miradi ya maendeleo inatarajiwa kubaki katika viwango vile vile katika kipindi cha muda wa kati kama inavyoonekana katika miradi na programu zinazoendelea.

(b) Sera ya Kugharamia Nakisi ya Bajeti

82. Kwa kuzingatia Mkakati wa kipindi cha Muda wa Kati wa Kusimamia Deni la Taifa wa mwaka 2017/18 – 2021/22, miradi ya maendeleo, hususan miradi mikubwa ya kimkakati itagharamiwa kwa kutumia fursa ya mikopo yenye masharti nafuu na masharti ya kati kwa kuzingatia wigo wa uhimilivu wa deni. Serikali itatumia mikopo yenye masharti ya wastani (*semi-concessional loans*) kugharamia miradi ya maendeleo ili kukabiliana na changamoto ya kupungua kwa upatikanaji wa mikopo yenye masharti nafuu, pamoja na kupunguza athari zinazoweza kutokea kwa kukopa ndani kwa kutumia dhamana za Serikali za muda mfupi.

3.3.6. Ukopaji kutoka Vyanzo vya Ndani

83. Ukopaji katika soko la ndani utaendelea kuwa chanzo muhimu cha kugharamia bajeti ya Serikali. Serikali itaendelea kukopa katika soko la ndani kwa kiwango ambacho hakitaathiri ukopaji wa sekta binafsi. Serikali imekua ikitekeleza hatua mbalimbali za kisera ili kukuza soko la fedha la ndani ambalo ni chanzo muhimu katika kugharamia bajeti. Hatua hizo za kisera ni pamoja na: kuboresha miundombinu ya soko la fedha, kuongeza wastani wa muda wa uivaji wa dhamana za Serikali na kufungua wigo kwa wawekezaji wa nje kununua dhamana za Serikali. Vile vile, ili kupunguza athari zinazoweza kujitokeza za kulipa madeni kwa utaratibu wa kukopa na kurejesha mikopo iliyoiva '*rollover*', Serikali imedhamiria

kupunguza sehemu ya Dhamana za Serikali za muda mfupi zinazoiva kwa kutumia Hatifungani za Serikali za muda wa kati na mrefu.

3.3.7. Ukopaji kutoka Vyanzo vya Nje

84. Serikali itaendelea kutumia mikopo ya masharti nafuu kama chanzo muhimu cha kuziba nakisi ya bajeti; mikopo yenye masharti ya kibiashara itakopwa kwa uangalifu na kuelekezwa kwenye miradi ya maendeleo yenye matokeo makubwa ya manufaa kiuchumi. Aidha, kukamilika kwa zoezi la tathmini ya uwezo wa nchi wa kukopa na kulipa madeni, kutaiwezesha Serikali kuuza hatifungani katika soko la fedha la kimataifa hatua ambayo itaongeza vyanzo vya ukopaji na hivyo kupunguza utegemezi katika soko la fedha la ndani.

3.3.8. Makadirio ya Kuziba Nakisi ya Bajeti

85. Katika kipindi cha muda wa kati, nakisi ya bajeti bila misaada, inakadiriwa kuwa Shilingi bilioni 4,286.9 mwaka 2019/20 (sawa na asilimia 2.7 ya Pato la Taifa) na kupungua hadi Shilingi bilioni 2,163.6 mwaka 2021/22 (sawa na asilimia 1.1 ya Pato la Taifa). Nakisi ya bajeti ikijumuisha misaada (*grants*) inakadiriwa kuwa Shilingi bilioni 2,943.6 (sawa na asilimia 1.9 ya Pato la Taifa) mwaka 2019/20 na inategemea kupungua hadi Shilingi bilioni 782.9 (sawa na asilimia 0.4 ya Pato la Taifa) mwaka 2021/22.

86. Kwa ujumla, nakisi ya bajeti itaendelea kupungua katika kipindi cha kati kutokana na; kukamilika kwa baadhi ya miradi mikubwa ya maendeleo sanjari na kufikiwa kwa kigezo cha utengamano wa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa kuwa na nakisi ya bajeti isiyozidi asilimia 3 ya Pato la Taifa.

Jedwali Na. 3.1: Mchanganuo wa Makadirio ya Bajeti Katika Kipindi cha Muda wa Kati 2019/20 – 2021/22

MAKADIRIO YA BAJETI KWA MWAKA 2018/19 - 2021/22 (Kwa Mchanganuo)				
				Shilingi Milioni
	2018/19	2019/20	2020/21	2021/22
	BAJETI ILIYOIDHINISHWA	MAKADIRIO YA BAJETI	MAKADIRIO YA BAJETI	MAKADIRIO YA BAJETI
Mapato ya Ndani (Ikijumuisha Mapato ya LGAs)	**20,894,578**	**23,206,831**	**25,726,273**	**28,113,887**
Mapato ya Ndani	**20,158,989**	**22,411,149**	**24,846,757**	**27,156,757**
Mapato ya kodi (TRA)	18,000,219	20,124,105	22,308,209	24,385,369
Mapato yasiyo ya kodi	2,158,770	2,287,045	2,538,548	2,771,389
Mapato ya Halmashauri	**735,589**	**795,682**	**879,516**	**957,130**
Jumla ya Matumizi	**26,206,296**	**27,493,740**	**28,860,089**	**30,277,440**
Matumizi ya Kawaida	14,199,023	15,109,339	15,973,137	16,717,601
Malipo ya Riba Nje	689,667	1,047,005	1,101,677	1,140,790
Malipo ya Riba Ndani	1,413,631	1,572,164	1,764,562	1,987,959
Mishahara	7,409,952	7,558,974	7,915,645	8,422,740
Michango ya Serikali kwenye Mifuko ya Jamii	1,195,866	1,273,090	1,407,226	1,531,407
Matumizi Mengine	**3,489,907**	**3,658,105**	**3,784,027**	**3,634,704**
Matumizi ya Maendeleo	**12,007,273**	**12,384,400**	**12,886,952**	**13,559,839**
Fedha za Ndani	9,876,393	9,555,672	10,110,157	10,836,658
Fedha za Nje	2,130,880	2,828,728	2,776,795	2,723,181
Nakisi ya Bajeti bila kujumuisha Misaada	**-5,311,718**	**-4,286,909**	**-3,133,816**	**-2,163,553**
Misaada	**1,081,408**	**1,343,324**	**1,361,800**	**1,380,674**
Misaada ya Kibajeti	236,264	238,717	242,000	245,354
Miradi ya Maendeleo	752,982	978,236	991,690	1,005,435
Mifuko ya Kisekta	92,163	126,371	128,109	129,885
Nakisi ya Bajeti ikiujumuisha Misaada	**-4,230,310**	**-2,943,585**	**-1,772,016**	**-782,879**
Jumla ya Nakisi	**-4,230,311**	**-2,943,585**	**-1,772,016**	**-782,880**
Kuziba Nakisi	**4,230,311**	**2,943,585**	**1,772,016**	**782,880**
Kuziba Nakisi kutoka Nje	**3,036,642**	**1,670,495**	**364,791**	**-748,528**
Mikopo Nafuu ya Kibajeti	309,501	312,714	317,016	321,409
Mikopo Nafuu ya Miradi ya Maendeleo	1,252,035	1,612,934	1,544,279	1,473,583
Mikopo Nafuu ya Mifuko ya Kisekta	33,701	111,187	112,717	114,279
Mikopo ya Kibiashara	3,111,058	1,737,303	1,408,958	952,324
Kulipa Mtaji Deni la Nje	-1,669,653	-2,103,644	-3,018,178	-3,610,122
Kuziba Nakisi kutoka Ndani	**1,193,669**	**1,273,090**	**1,407,226**	**1,531,408**
Mikopo ya Kibenki na isiyo ya kibenki	**1,193,669**	**1,273,090**	**1,407,226**	**1,531,408**
Kulipa Mtaji Deni la Ndani (Rollover)	4,600,000	3,902,795	3,871,346	4,284,894
Kulipa Mtaji Deni la Ndani (Rollover)	-4,600,000	-3,902,795	-3,871,346	-4,284,894
memo:				
GDPmp	**144,055,003**	**158,484,120**	**173,917,825**	**189,086,085**

Jedwali Na. 3.2: Mchanganuo wa Makadirio ya Bajeti Kwa Asilimia ya Pato Ghafi la Taifa kwa Kipindi cha Muda wa Kati 2019/20 – 2021/22

MAKADIRIO YA BAJETI KWA MWAKA 2018/19 - 2021/22 (Kwa Mchanganuo) KWA % GDP				
	2018/19	2019/20	2020/21	2021/22
	BAJETI ILIYOIDHINISHWA	MAKADIRIO YA BAJETI	MAKADIRIO YA BAJETI	MAKADIRIO YA BAJETI
Mapato ya Ndani (Ikijumuisha Mapato ya LGAs)	14.5%	14.6%	14.8%	14.9%
Mapato ya Ndani	14.0%	14.1%	14.3%	14.4%
Mapato ya kodi (TRA)	12.5%	12.7%	12.8%	12.9%
Mapato yasiyo ya kodi	1.5%	1.4%	1.5%	1.5%
Mapato ya Halmashauri	0.5%	0.5%	0.5%	0.5%
Jumla ya Matumizi	18.2%	17.3%	16.6%	16.0%
Matumizi ya Kawaida	9.9%	9.5%	9.2%	8.8%
Malipo ya Riba Nje	0.5%	0.7%	0.6%	0.6%
Malipo ya Riba Ndani	1.0%	1.0%	1.0%	1.1%
Mishahara	5.1%	4.8%	4.6%	4.5%
Michango ya Serikali kwenye Mifuko ya Jamii	0.8%	0.8%	0.8%	0.8%
Matumizi Mengine	2.4%	2.3%	2.2%	1.9%
Matumizi ya Maendeleo	8.3%	7.8%	7.4%	7.2%
Fedha za Ndani	6.9%	6.0%	5.8%	5.7%
Fedha za Nje	1.5%	1.8%	1.6%	1.4%
Nakisi ya Bajeti bila kujumuisha Misaada	-3.7%	-2.7%	-1.8%	-1.1%
				0.0%
Misaada	0.8%	0.8%	0.8%	0.7%
Misaada ya Kibajeti	0.2%	0.2%	0.1%	0.1%
Miradi ya Maendeleo	0.5%	0.6%	0.6%	0.5%
Mifuko ya Kisekta	0.1%	0.1%	0.1%	0.1%
		0.0%	0.0%	0.0%
Nakisi ya Bajeti ikiujumuisha Misaada	-2.9%	-1.9%	-1.0%	-0.4%
Jumla ya Nakisi	-2.9%	-1.9%	-1.0%	-0.4%
Kuziba Nakisi	2.9%	1.9%	1.0%	0.4%
Kuziba Nakisi kutoka Nje	2.1%	1.1%	0.2%	-0.4%
Mikopo Nafuu ya Kibajeti	0.2%	0.2%	0.2%	0.2%
Mikopo Nafuu ya Miradi ya Maendeleo	0.9%	1.0%	0.9%	0.8%
Mikopo Nafuu ya Mifuko ya Kisekta	0.0%	0.1%	0.1%	0.1%
Mikopo ya Kibiashara	2.2%	1.1%	0.8%	0.5%
Kulipa Mtaji Deni la Nje	-1.2%	-1.3%	-1.7%	-1.9%
Kuziba Nakisi kutoka Ndani	0.8%	0.8%	0.8%	0.8%
Mikopo ya Kibenki na isiyo ya kibenki	0.8%	0.8%	0.8%	0.8%
Kulipa Mtaji Deni la Ndani (Rollover)	3.2%	2.5%	2.2%	2.3%
Kulipa Mtaji Deni la Ndani (Rollover)	-3.2%	-2.5%	-2.2%	-2.3%
memo:				
GDPmp	**144,055,003**	**158,484,120**	**173,917,825**	**189,086,085**

Jedwali Na. 3.3: Makadirio ya Bajeti Katika Kipindi cha Muda wa Kati 2019/20 – 2021/22

Makadirio ya Bajeti 2018/19 - 2021/22 (shilingi milioni)				
	2018/19 BAJETI ILIYOIDHINISHWA	2019/20 MAKADIRIO YA BAJETI	2020/21 MAKADIRIO YA BAJETI	2021/22 MAKADIRIO YA BAJETI
I. JUMLA YA MAPATO	**32,475,949**	**33,500,179**	**35,749,613**	**38,172,457**
Mapato ya Ndani	20,158,989	22,411,149	24,846,757	27,156,757
Mapato ya Halmashauri	735,589	795,682	879,516	957,130
Misaada na Mikopo Nafuu ya Kibajeti	545,765	551,431	559,016	566,764
Misaada na Mikopo Nafuu ya Miradi	2,005,016	2,591,170	2,535,969	2,479,018
Mifuko ya Kisekta	125,864	237,558	240,826	244,163
Kulipa Mtaji Deni la Ndani (Rollover)	4,600,000	3,902,795	3,871,346	4,284,894
Mikopo ya Ndani ya Kibiashara	1,193,669	1,273,090	1,407,226	1,531,408
Mikopo ya Nje ya Kibiashara	3,111,058	1,737,303	1,408,958	952,324
II. JUMLA YA MATUMIZI	**32,475,949**	**33,500,179**	**35,749,613**	**38,172,457**
MATUMIZI YA KAWAIDA	20,468,676	21,115,779	22,862,661	24,612,618
Mfuko Mkuu wa Serikali	10,004,480	10,376,108	11,690,699	13,129,451
Mishahara	7,409,952	7,558,974	7,915,645	8,422,740
Matumizi Mengineyo	3,054,244	3,180,696	3,256,318	3,060,426
MATUMIZI YA MAENDELEO	12,007,273	12,384,400	12,886,952	13,559,839
Fedha za Ndani	9,876,393	9,555,672	10,110,157	10,836,658
Fedha za Nje	2,130,880	2,828,728	2,776,795	2,723,181

Jedwali Na. 3.4: Makadirio ya Bajeti kwa Asilimia ya Pato Ghafi la Taifa Kwa Kipindi cha Muda wa Kati 2019/20 – 2021/22

Makadirio ya Bajeti kwa Mwaka 2018/19 - 2021/22 kwa % ya Bajeti Nzima				
	2018/19 BAJETI ILIYOIDHINISHWA	2019/20 MAKADIRIO YA BAJETI	2020/21 MAKADIRIO YA BAJETI	2020/21 MAKADIRIO YA BAJETI
I. JUMLA YA MAPATO	**100%**	**100%**	**100%**	**100%**
Mapato ya Ndani	62.1%	66.9%	69.5%	71.1%
Mapato ya Halmashauri	2.3%	2.4%	2.5%	2.5%
Misaada na Mikopo Nafuu ya Kibajeti	1.7%	1.6%	1.6%	1.5%
Misaada na Mikopo Nafuu ya Miradi	6.2%	7.7%	7.1%	6.5%
Mifuko ya Kisekta	0.4%	0.7%	0.7%	0.6%
Kulipa Mtaji Deni la Ndani (Rollover)	14.2%	11.7%	10.8%	11.2%
Mikopo ya Ndani ya Kibiashara	3.7%	3.8%	3.9%	4.0%
Mikopo ya Nje ya Kibiashara	9.6%	5.2%	3.9%	2.5%
II. JUMLA YA MATUMIZI	**100%**	**100%**	**100%**	**100%**
MATUMIZI YA KAWAIDA	**63.0%**	**63.0%**	**64.0%**	**64.5%**
Mfuko Mkuu wa Serikali	**30.8%**	**31.0%**	**32.7%**	**34.4%**
Mishahara	**22.8%**	**22.6%**	**22.1%**	**22.1%**
Matumizi Mengineyo	**9.4%**	**9.5%**	**9.1%**	**8.0%**
MATUMIZI YA MAENDELEO	**37.0%**	**37.0%**	**36.0%**	**35.5%**
Fedha za Ndani	30.4%	28.5%	28.3%	28.4%
Fedha za Nje	6.6%	8.4%	7.8%	7.1%

3.4. Vipaumbele katika Kipindi cha Muda wa Kati

87. Katika kipindi cha muda wa kati, Serikali itaendelea kutekeleza Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2016/17 – 2020/21 kwa kuzingatia maeneo makuu manne ya kipaumbele ambayo ni: Kukuza Uchumi na Ujenzi wa Msingi wa Uchumi wa Viwanda; Kufungamanisha Uchumi na Maendeleo ya Watu; Kujenga Mazingira Wezeshi kwa Uendeshaji wa Biashara na Uwekezaji; na Kuboresha Utekelezaji wa Mpango.

3.4.1. Kukuza Uchumi na Ujenzi wa Msingi wa Uchumi wa Viwanda

88. Katika kipindi cha muda wa kati, mkakati utalenga kutekeleza miradi ya kimkakati ambayo itakuwa na matokeo makubwa katika sekta nyingine za kiuchumi. Miradi hiyo ni pamoja na: Ujenzi wa Bomba la kusafirisha Mafuta ghafi kutoka Hoima (Uganda) hadi Tanga (Tanzania); Kuboresha Shirika la Ndege Tanzania (ATCL); Ujenzi wa reli mpya ya kati kwa kiwango cha *Standard Gauge;* Kusomesha kwa wingi Rasilimali Watu katika fani na Ujuzi Adimu na Maalum kwa Maendeleo ya Viwanda na Watu; Uanzishwaji wa Maeneo Maalum ya Kiuchumi; Shamba la Miwa na Kiwanda cha Sukari Mkulazi; na Kuzalisha Umeme kwa nguvu za Maji katika Bonde la Mto Rufiji. Maeneo mengine ni Viwanda, Kilimo, Madini, Mifugo, Uvuvi, Misitu, Wanyamapori, Utalii, Biashara na Masoko.

3.4.2. Maendeleo ya Watu

89. Vipaumbele katika kipindi cha muda wa kati vinajumuisha:

(i) **Elimu:** Kuimarisha utoaji wa elimu ya awali, msingi na sekondari; kuendelea kutoa elimumsingi bila ada; kuboresha ukaguzi wa shule; kuimarisha utoaji wa elimu ya ufundi; kuboresha ukaguzi na kuongeza matumizi ya TEHAMA katika vyuo vya mafunzo ya ufundi na ualimu; kuimarisha utoaji wa elimu ya juu kwa kuongeza upatikanaji wa mikopo kwa wanafunzi, matumizi ya TEHAMA kufundishia na kujifunzia, ujenzi na ukarabati wa miundombinu katika vyuo vya elimu ya juu.

(ii) **Afya:** Kuboresha mfumo wa rufaa na kuimarisha upatikanaji wa huduma za kibingwa kwa kuwezesha hospitali za rufaa za mikoa, kanda na kitaifa ikiwa ni pamoja na kusimika vifaa tiba vya kisasa na mafunzo kwa wataalam; kusimika vifaa tiba vya kisasa katika hospitali zote maalum; ujenzi na ukarabati wa vyuo vya afya na miundombinu mingine; na utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Lishe.

(iii) **Maji na Usafi wa Mazingira:** Kusimamia vyanzo vya maji na kudhibiti ubora; Ujenzi wa mabwawa ya maji; Kuboresha usambazaji maji mijini na vijijini; na uboreshaji wa miundombinu ya maji taka.

(iv) **Ajira:** Kuongeza fursa za ajira; kuimarisha Mfuko wa Maendeleo ya Vijana; kutoa mafunzo katika ujuzi unaohitajika kwenye soko la ajira; kukuza

uadilifu na utamaduni wa kufanya kazi kwa bidii kwa waajiriwa; kuhamasisha ari ya ubunifu na ujasiriamali; kutenga maeneo maalum ya uwekezaji, shughuli za kibiashara na vituo atamizi, na kuhamasisha programu maalum za mafunzo.

(v) **Uwezeshaji Kiuchumi:** Kuongeza ushiriki wa wananchi katika shughuli za kiuchumi.

(vi) **Utawala bora na Huduma Kwa Wananchi:** kuendelea kuongeza ufanisi katika utoaji huduma za kisheria na haki kwa wananchi kupitia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Mashtaka ya Taifa na Wakili Mkuu wa Serikali.

3.4.3. Kuboresha Mazingira ya kufanya Biashara na Uwekezaji

90. Katika kipindi cha muda wa kati, Serikali itaendelea kutekeleza sera madhubuti za fedha na bajeti ili kuwa na utulivu wa uchumi jumla. Serikali itaendelea kuboresha mazingira ya kufanya biashara na uwekezaji kama ilivyobainishwa kwenye andiko la *Blueprint*. Aidha, Serikali itajielekeza katika kuboresha mifumo ya kisera, kisheria na udhibiti katika biashara; kufuta na kupunguza baadhi ya ada na tozo kero; kuboresha miundombinu ya reli, barabara, nishati, viwanja vya ndege na bandari; kukarabati na kununua meli mpya za abiria na mizigo; kununua na kukarabati vivuko; kuimarisha mifumo ya TEHAMA, upanuzi wa mtandao wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano, na utekelezaji wa mfumo wa kitaifa wa kielektroniki ili kuharakisha uondoaji wa mizigo bandarini.

3.4.4. Kuboresha Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano

91. Katika kuboresha utekelezaji wa shughuli za mipango na bajeti, Serikali itaendelea kutekeleza maboresho ya mifumo na taratibu mbalimbali za ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji. Mikakati mbalimbali ya kuboresha utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano imeainishwa katika Mkakati wa Utekelezaji wa Mpango huo ambayo ni: Kutekeleza maboresho yanayohusiana na utawala bora, utawala wa sheria, utoaji wa haki, ulinzi na usalama na udhibiti wa rushwa; kukuza utamaduni wa kufanya kazi kwa bidii; kuboresha mazingira ya biashara; kuwezesha utekelezaji wa miradi ya kimkakati; kuboresha usimamizi wa ardhi; kurasimisha sekta isiyo rasmi pamoja na kuhamasisha maendeleo ya wazawa.

SURA YA NNE

VIHATARISHI VYA KIBAJETI KATIKA MUDA WA KATI

4.1. Utangulizi

92. Vihatarishi vya kibajeti ni matukio ambayo yanaweza kusababisha matokeo ya utekelezaji wa bajeti ya Serikali kutofikia malengo yaliyotarajiwa katika muda wa kati au kuathiri uendelevu wake katika muda mrefu. Matukio hayo yanaweza kuathiri utekelezaji na usimamizi wa Bajeti ya Serikali kama hakutakuwa na juhudi madhubuti za kuyadhibiti. Hivyo, mafanikio ya malengo ya bajeti yatategemea uwezo wa Serikali wa kubainisha, kutathmini na kukabiliana na matukio hayo.

93. Katika kuandaa bajeti ya muda wa kati, Serikali inazingatia vigezo vikuu vya viashiria vya uchumi jumla ikiwa ni pamoja na uwiano wa nakisi ya bajeti kwa Pato la Taifa na uhimilivu wa deni la Taifa. Kwa miaka ya hivi karibuni, Serikali imeshuhudia matokeo ya utekelezaji yalikuwa chini ya malengo yaliyotarajiwa, ukuaji wa uchumi usioendana na maoteo, mtikisiko wa bei katika masoko ya nje (kama mabadiliko ya bei za mafuta); mabadiliko ya viwango vya kubadilisha fedha, majanga asilia; madai ya malipo kutokana na udhamini wa Serikali kwa Taasisi za Serikali na Mashirika ya Umma ambayo yameshindwa kulipa mikopo iliyodhaminiwa; na madai mengine mbalimbali yasiyotarajiwa.

94. Sheria ya Bajeti, SURA 439 inaelekeza Serikali kusimamia na kukabiliana na vihatarishi vya kibajeti ili kufikia malengo ya uchumi jumla ya muda wa kati. Tathmini na uelewa wa kina kuhusu vyanzo, ukubwa na uwezekano wa vihatarishi vya kibajeti kutokea ni muhimu katika kuhakikisha Serikali inatimiza malengo yake ya kibajeti na kuepukana na madhara ya mabadadiliko ya sera yasiyo ya lazima wakati wa utekelezaji wa bajeti. Hivyo, usimamizi madhubuti wa vihatarishi ni muhimu katika kulinda rasilimali za umma. Sura hii imeainisha maeneo yanayoweza kuwa chanzo cha vihatarishi kwenye utekelezaji wa bajeti, na hivyo kupelekea Serikali kutofikia malengo ya mapato na matumizi kwa muda wa kati. Aidha, hatua ambazo Serikali inaweza kuchukua kukabiliana na vihatarishi hivyo zimebainishwa.

4.2. Maeneo ya Vihatarishi

(a) Ukuaji wa Pato la Taifa

95. Pato la Taifa ni chanzo cha msingi kwa ukusanyaji wa mapato ya kodi. Kilimo ambacho huchangia Pato la Taifa kwa takriban asilimia 30, kinakua kwa kasi ndogo na hivyo kuathiri upatikanaji wa mapato yakutosha na endelevu. Ukuaji wa

kuridhisha wa sekta ya Kilimo utategemea uwezo wa Serikali wa kusimamia vihatarishi vinavyohusiana na sekta hiyo (kama vile hali mbaya ya hewa; mlipuko wa wadudu wanaoharibu mazao; mabadiliko makubwa ya bei za pembejeo za kilimo zinazozalishwa ndani ya nchi na zile zinazoagizwa nje ya nchi).

(b) Mabadiliko ya Viwango vya Kubadilisha Fedha

96. Serikali imekuwa ikilipa mihadi ya madeni yake ya nje kwa wakati na kwa kuzingatia bajeti. Mabadiliko yasiyotarajiwa ya viwango vya kubadilisha fedha, mfano kutokana na kushuka kwa thamani ya Shilingi ya Tanzania, yatailazimu Serikali kutumia fedha nyingi zaidi kulipa madeni yake ya nje. Aidha, kwa kuwa Serikali huagiza bidhaa nyingi zaidi kutoka nje kuliko inavyouza nje, kushuka kwa thamani ya Shilingi kunaweza kuongeza gharama za utekelezaji wa miradi muhimu ya miundombinu ambayo hutegemea zaidi vifaa vinavyoagizwa nje ya nchi.

(c) Misaada na Mikopo

97. Bajeti ya Serikali hutegemea misaada na mikopo kutoka nje. Hali hii hufanya utekelezaji wa bajeti kuwa katika hali hatarishi kwa kutofikiwa kwa malengo ya bajeti pale misaada na mikopo inapopungua, kutopatikana kwa wakati au kupanda kwa gharama za mikopo.

(d) Mabadiliko ya Bei za Bidhaa

98. Mabadiliko ya bei za bidhaa katika soko la dunia huathiri utekelezaji wa bajeti. Kushuka kwa bei za bidhaa za dhahabu na bidhaa asilia kunaweza kupunguza mapato yatokanayo na mauzo ya nje ya nchi na kunaweza kusababisha ongezeko la nakisi ya bajeti katika akaunti ya biashara na kupunguza akiba ya fedha za kigeni. Aidha, kuongezeka kwa bei za bidhaa kutoka nje hususan bidhaa za mafuta kunaweza kuongeza gharama za kupata bidhaa na huduma za ndani na hivyo kusababisha kushindwa kufikiwa malengo ya mapato na matumizi katika muda wa kati.

(e) Matumizi ya Serikali

99. Taarifa za hivi karibuni za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali zimebainisha uwepo wa udhibiti mdogo wa matumizi ya fedha za Serikali. Kuendelea kujitokeza kwa hali hii kutahatarisha utekelezaji wa bajeti na kusababisha ongezeko la madai kwa Serikali na mabadiliko ya vipaumbele vya bajeti. Malimbikizo ya madai yanaweza kuathiri ufanisi wa biashara za sekta binafsi kwa kukwamisha upanuzi na kupunguza faida na hivyo kupunguza mapato ya kodi.

(f) Madeni Sanjari

100. Madeni sanjari yanaweza kuathiri kwa kiasi kikubwa utekelezaji wa bajeti katika muda wa kati. Usimamizi usioridhisha wa madeni sanjari yanayotokana na udhamini wa mikopo kwa Mashirika na Taasisi nyingine za Serikali pamoja na tuzo za mahakama kunaweza kusababisha Serikali kushindwa kufikia malengo ya muda wa kati ya mapato na matumizi. Hali kadhalika, tathmini isiyotosheleza ya madeni sanjari inaweza kuingiza Serikali katika madai makubwa yasiyotarajiwa katika muda mfupi, wa kati na mrefu na kusababisha uhitaji mkubwa wa rasilimali fedha.

(g) Majanga ya Asili

101. Vihatarishi vinavyotokana na mabadiliko ya tabianchi kama vile mafuriko, ukame, maporomoko ya ardhi, matetemeko na majanga mengine ya asili husababisha kukwama kwa shughuli za kiuchumi, uharibifu wa miundombinu na uhaba wa bidhaa na huduma. Urejeshwaji wa miundombinu ya kiuchumi iliyoharibika kutokana na majanga hayo huhitaji bajeti ya ziada nje ya bajeti iliyopangwa. Aidha, kuharibika kwa miundombinu hiyo kunaweza kuwa na madhara mengine ya kiuchumi kama vile kuongezeka kwa mfumuko wa bei, kuongezeka kwa gharama za uzalishaji viwandani; kupungua kwa faida za kampuni na hivyo kusababisha upungufu katika ukusanyaji wa mapato na kupanua nakisi ya Bajeti.

(h) Ulipaji wa Madeni

102. Mikopo ya ndani ni moja ya vyanzo vinavyotumiwa na Serikali kugharamia nakisi ya bajeti. Sehemu ya mikopo hiyo hukopwa kutoka katika soko la ndani kupitia mauzo ya dhamana za serikali. Dhamana zinapoiva, Serikali huhitaji kukopa tena katika soko la ndani kulipa madeni hayo. Vihatarishi vya malipo ya madeni hutokea pale Serikali inapokosa kiasi cha mikopo inayohitajika kutoka kwenye masoko ya fedha ya ndani au gharama za kukopa katika soko zinapokuwa juu kuliko ilivyotarajiwa. Hali hii inaweza kusababisha Serikali kushindwa kulipa madeni yake na hivyo kuongeza mzigo wa madeni.

4.3. Hatua za Kukabiliana na Vihatarishi

(a) Udhibiti wa Matumizi ya Serikali

103. Katika muda wa kati, mkazo utawekwa katika kuimarisha Sera za usimamizi wa fedha na udhibiti wa matumizi katika ngazi zote za Serikali kwa kuzingatia Sheria ya Fedha za Umma SURA 348, Sheria ya Bajeti, SURA 439, Sheria ya Ununuzi wa Umma SURA 410, Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa SURA 290 na Kanuni zake pamoja na nyaraka nyingine za Serikali.

104. Aidha, juhudi zitafanywa ili kuendelea kujenga nidhamu ya matumizi katika ngazi zote za Serikali na kuhakikisha kwamba matumizi yanafanyika kulingana na mipango na vipaumbele vya Serikali na kwa kuzingatia upatikanaji wa fedha. Serikali itachukua hatua za kisheria na za kinidhamu kwa watumishi watakaobainika kwenda kinyume na taratibu kwa mujibu wa Kanuni za Adhabu za mwaka 2005.

(b) Udhibiti wa Utoaji Dhamana

105. Katika kuhakikisha kunakuwa na tathmini ya kutosha ya vihatarishi vinavyohusiana na dhamana, Serikali itafuatilia kwa karibu madeni sanjari kwa kuongeza usimizi wa utekelezaji wa Sera za utoaji dhamana. Serikali itafuatilia kwa makini madhumuni na vigezo vya utoaji wa dhamana kwa mujibu wa Sheria ya Mikopo, Misaada na Dhamana, SURA 134, na Mkakati wa Muda wa Kati wa Madeni ili kufikia lengo la Serikali la kupunguza nakisi ya bajeti.

(c) Usimamizi wa Majanga

106. Vihatarishi vinavyotokana na matukio ya maafa vitazingatiwa kikamilifu kwa kuongeza ufanisi katika utabiri wa hali ya hewa na utekelezaji wa Muundo wa Usimamizi wa Maafa ulio chini ya Idara ya Usimamizi wa Maafa katika Ofisi ya Waziri Mkuu. Aidha, katika kipindi cha muda wa kati, Serikali imedhamiria kujenga skimu za kimkakati za umwagiliaji na mabwawa ili kudhibiti athari zinazoweza kutokea kutokana na ukame na kuhakikisha uzalishaji endelevu wa kilimo na usalama wa chakula. Vile vile, Serikali itaendelea kutenga fedha katika Mfuko wa Dharura ili kukabiliana na majanga ya maafa na kuweka Kanuni na Mwongozo kwa ajili ya usimamizi wa maafa.

(d) Usimamizi wa Vihatarishi vya Misaada na Mikopo

107. Serikali kupitia Kamati ya Usimamizi wa Soko la Hati Fungani imeandaa Mpango wa Serikali wa Utoaji na Usimamizi wa Mauzo ya Dhamana za Serikali kwenye soko la fedha ili kuhakikisha kuwa kunakuwa na ulinganifu na mpangilio mzuri wa utoaji wa Dhamana, Hati Fungani na nyenzo nyingine za mikopo kwa ajili ya kugharamia bajeti ya Serikali. Serikali imedhamiria kuzingatia kikamilifu Mpango huo.

108. Serikali itachukua hatua zaidi kuimarisha biashara, ukwasi na ufanisi katika soko la dhamana. Aidha, Serikali itafanya marekebisho ya Sheria ili kuhakikisha kuwa akaunti ya dhamana inakuwa huru kwa wadau mbalimbali, lengo likiwa ni kufungua fursa za biashara ya dhamana kwa wawekezaji wengi zaidi kutoka ukanda wa Afrika Mashariki na sehemu nyingine duniani. Ili kufanikisha azma hii, Serikali itachukua tahadhari ili kuhakikisha kuwa soko la mitaji linabaki kuwa imara

wakati wote.

109. Vile vile, Serikali itachukua hatua ili kuongeza tija katika ukusanyaji wa mapato ya ndani ikiwa ni pamoja na kupanua wigo wa kodi. Juhudi hizo ni pamoja na kufanya kilimo kuwa cha kisasa ili kichangie katika kuongeza wigo wa kodi, kwa kuongeza thamani ya mazao ya kilimo ili kufikia azma ya Serikali ya kujenga uchumi wa viwanda.

110. Serikali inaendelea kuboresha mazingira ya kufanya biashara ili kuimarisha ubia kati ya Serikali na sekta binafsi katika kuchangia, kusimamia na kuimarisha utoaji wa huduma kwa umma ili kupunguza mzigo katika bajeti ya Serikali kwa shughuli ambazo zinaweza kufanywa kwa ubia.

(e) Soko la Bidhaa

111. Soko la Bidhaa ni mahali rasmi ambapo wakulima, wafanyabiashara, wauzaji na wanunuzi wa bidhaa na wadau wengine mbalimbali hukutana kwa lengo la kutafuta masoko ya ndani na nje ili kupata bei halisi ya kuuza au kununua bidhaa. Katika Soko la Bidhaa, wauzaji na wanunuzi hufanya biashara, huwa na uhakika wa kupata mazao waliyonunua yakiwa na ubora na kwa kiasi kilichokubalika, uhakika wa malipo na ukakika wa bidhaa iliyonunuliwa kufika kwa mnunuzi. Soko la Bidhaa limehuishwa na Mfumo wa Stakabadhi za Mazao Ghalani kwa kuhakikisha kuwa mazao yaliyopo ghalani yanapata bei sahihi ili kuwalinda wakulima dhidi ya hasara inayoweza kutokea kutokana na udhalimu wa soko au kuuza mazao kwa bei isiyostahili kutokana na kukosa taarifa sahihi za bei ya soko.

112. Bidhaa zitakazopewa kipaumbele katika Soko la Bidhaa ni Mahindi, Mbaazi, Mkonge, Chai, Mifugo na Tumbaku. Bidhaa nyingine ni pamoja na Ufuta, Alizeti, Korosho, Njugu Mawe, soya, Pamba, Mchele na madini kama vile Dhahabu na Shaba.

Overview of Expenditure by Divisions and Groups of CoFOG

Government Broad Objective (Division)	Sub-items (Groups)	Medium Term Projections (Millions)		
		2019/20	2019/21	2019/22
General public services	Executive and legislative organs, financial and fiscal affairs, external affairs; general services; basic research; R&D related to general public services; general public services not elsewhere classified; public debt transactions, transfers of a general character between different levels of Government.	14,560.66	15,455.74	16,968.16
Economic affairs	General economic, commercial and labour affairs; agriculture, forestry; fishing and hunting; fuel and energy; mining, manufacturing and construction; transport; communication; other industries, R&D related to economic affairs; economic affairs not elsewhere classified	7,799.51	8,323.23	8,887.34
Education	Pre-primary, primary, secondary and tertiary education, post-secondary non-tertiary education, education non-definable by level, subsidiary services to education, R&D; not elsewhere classified.	4,787.91	5,109.34	5,455.72
Defence	Military defence; civil defence; R&D related to defence; defence not elsewhere classified.	2,016.8	2,178.5	2,346.5
Health	Medical products, appliances and equipment; outpatient services; hospital services; public health services; R&D related to health; health not elsewhere classified.	1,847.2	1,995.3	2,149.1
Public order and safety	Police services; fire-protection services; law courts; prisons; R&D related to public order and safety; public order and safety not elsewhere classified.	1,203.3	1,299.8	1,400.0
Housing and community amenities	Housing development; community development; water supply; street lighting; R&D related to housing and community amenities; housing and community amenities not elsewhere classified.	1,086.5	1,173.6	1,264.1
Social protection	Sickness and disability; old age; survivors; family and children; unemployment; housing; R&D; social protection and social exclusion not elsewhere classified.	135.8	146.6	157.9
Sports,	Recreational and sporting services;	34.6	37.4	40.3

Government Broad Objective (Division)	Sub-items (Groups)	Medium Term Projections (Millions)		
		2019/20	2019/21	2019/22
Recreation and culture	cultural services; broadcasting and publishing services; other community services, R&D related to sports, recreation and culture; sports; recreation and culture not elsewhere classified.			
Environmental protection	Waste management; water waste management; pollution abatement; protection of biodiversity and landscape; R&D related to environmental protection.	27.9	30.1	32.4
CoFOG	**GRAND TOTAL**	**33,500.18**	**35,749.61**	**38,172.46**

TAARIFA YA UKUSANYAJI WA MADUHULI KWA WIZARA/IDARA KWA MWAKA 2017/18

FUNGU	WIZARA/IDARA	Shilingi Milioni		
		BAJETI ILIYOIDHINISHWA	MAKUSANYO HALISI	ASILIMIA
48	Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi	112,047.21	92,155.41	82
65	Ajila na Kazi	35,029.61	30,929.54	88
93	Mambo ya Ndani- Idara ya Uhamiaji	180,800.00	159,263.76	88
99	Mifugo na Uvuvi	36,105.37	41,546.46	115
58	Nishati na Madini	727,502.00	607,460.54	83
28	Mambo ya Ndani -Jeshi la Polisi	73,645.42	78,908.02	107
29	Mambo ya Ndani - Jeshi la Magereza	2,650.00	2,187.66	83
37	Ofisi ya Waziari Mkuu- Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali	1,000.00	640.37	64
7	Msajili wa Hazina	529,582.94	803,502.12	152
44	Viwanda, Biashara na Uwekezaji	28,000.01	12,165.41	43
14	Mambo ya Ndani- Jeshi la Zimamoto na Uokoaji	35,550.00	6,404.18	18
43	Kilimo	2,015.01	2,276.46	113
69	Maliasili na Utalii	21,289.30	16,414.61	77
96	Habari Michezo na Utamaduni	1,574.61	837.37	53
34	Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa	25,773.48	29,372.03	114
40	Mfuko wa Mahakama	9,318.37	11,194.36	120
46	Elimu, Sayansi na Teknolojia	112,726.24	184,648.55	164
45	Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi	12,001.04	12,285.97	102
53	Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto - Maendeleo ya Jamii	2,099.87	2,521.76	120
52	Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto - Afya	17,815.77	12,714.86	71
62	Ujenzi Uchukuzi na Mawasiliano - Uchukuzi (TAA & TPA)	215,963.92	104,290.94	48
50	Fedha na Mipango	27.04	51.88	192
49	Maji	590.01	194.32	33
	Wizara nyingine	252.12	440.79	175
	JUMLA	**2,183,359.34**	**2,212,407.38**	**101**

UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MWAKA 2017/18 KWA MAFUNGU

A. MATUMIZI YA KAWAIDA

Vote Code	Vote Description	Revised Budget	Total Actual Expenditure	Actual Exp. As A % Of Annual Targets
002	Teachers Service Commission	12,506,678,758	9,426,463,452	75.4
003	National Land Use and Planning Commission	2,356,178,301	1,854,584,666	78.7
004	Records and Archives Management Department	3,202,349,180	2,242,470,872	70.0
005	National Irrigation Commission	4,055,481,000	3,869,888,870	95.4
007	The Treasury Registrar	29,651,900,087	14,474,469,221	48.8
009	Secretariat of Public Remunaration	1,721,987,000	1,414,288,358	82.1
010	Joint Finance Commision	1,452,741,955	1,183,247,860	81.4
011	Oil and Gas Bureau	711,073,000	-	-
012	Judicial Service Commission	1,124,528,995	857,729,007	76.3
013	Financial Intelligence Unit	1,515,586,000	1,471,962,558	97.1
014	Fire and Rescue Force	32,946,692,000	28,696,358,029	87.1
015	Commission for Mediation and Arbitration	3,412,791,000	2,639,608,217	77.3
016	Attorney General's Office	15,174,609,480	14,171,173,622	93.4
018	UNESCO Commission	663,123,000	281,355,300	42.4
020	State House	17,548,548,613	14,202,170,118	80.9
021	The Treasury	551,948,114,401	541,858,817,113	98.2
022	Public Debt and General Services	9,572,208,362,000	9,532,793,655,540	99.6
023	Accountant General's Department	69,103,595,951	65,323,614,790	94.5
024	The Cooperative Development Commission	6,578,412,249	5,498,916,446	83.6
025	Prime Minister	6,036,351,537	5,567,490,585	92.2
026	Vice President	8,261,628,114	7,817,467,470	94.6
027	Registrar of Political Parties	21,476,055,816	20,052,573,529	93.4
028	Ministry of Home Affairs - Police Force	631,664,450,920	608,574,529,285	96.3
029	Ministry of Home Affairs - Prisons Services	226,850,313,288	217,724,232,182	96.0
030	President's Office and Cabinet Secretariat	465,709,999,729	411,940,407,430	88.5
031	Vice President's Office	14,071,978,503	12,820,022,222	91.1
032	President's Office - Public Service Management and Good Governance	30,757,741,982	29,914,254,484	97.3
033	Ethics Secretariat	7,707,984,059	6,411,158,721	83.2
034	Ministry of Foreign Affairs and International Co-operation	154,239,589,923	131,901,848,272	85.5
035	Public Prosecution Division	16,391,089,042	14,592,869,586	89.0
036	RAS Katavi	57,472,286,780	42,379,380,356	73.7
037	Prime Minister's Office	24,299,938,821	17,515,547,497	72.1
038	Defence	1,294,059,869,835	1,285,083,033,129	99.3
039	National Service	331,104,874,213	327,367,070,101	98.9
040	The Judiciary Fund	107,048,053,522	85,697,609,764	80.1
041	Ministry of Constitutional Affairs and Justice	9,747,572,729	9,253,495,562	94.9
042	The National Assembly Fund	120,020,533,045	119,515,625,035	99.6
043	Ministry of Agriculture, Livestock Development and Fisheries - Agriculture Sector	65,779,147,982	54,236,814,917	82.5
044	Ministry of Industry, Trade and Investment	25,427,195,435	18,886,290,332	74.3
045	National Audit Office	63,312,666,876	50,483,624,470	79.7
046	Ministry of Education, Science and Tehcnology	435,207,798,884	425,383,712,460	97.7
047	RAS Simiyu	133,776,347,729	107,775,644,003	80.6
048	Ministry of Lands,Housing and Human Settlements Development	50,596,223,209	29,753,194,275	58.8
049	Ministry of Water and Irrigation	44,600,001,615	39,842,104,365	89.3
050	Ministry of Finance and Planning	71,931,122,975	62,557,194,403	87.0
051	Ministry of Home Affairs	24,243,774,566	22,887,245,710	94.4
052	Ministry of Health, Community Development, Gender, Elderly and Children - Health	324,984,273,930	276,852,535,408	85.2
053	Ministry of Health, Community Development, Gender, Elderly and Children	35,827,310,567	21,031,650,695	58.7
054	RAS Njombe	120,617,972,400	97,698,438,623	81.0
055	Commission for Human Rights and Good Governance	4,171,838,695	3,963,129,959	95.0
056	President's Office - Regional Administration and Local Government Authorities	42,157,582,286	39,005,405,087	92.5
057	Ministry of Defence and National Service	19,427,724,579	15,770,989,517	81.2
058	Ministry of Energy and Minerals	60,279,081,238	46,818,643,621	77.7
059	Law Reform Commission	2,234,264,006	1,943,135,848	87.0
060	Trade and Investment	19,257,539,750	12,543,137,647	65.1
061	Electoral Commission	10,124,133,690	8,860,029,796	87.5
062	Ministry of Works, Transport and Communication - Tansport	120,005,758,430	116,685,724,263	97.2
063	RAS Geita	164,854,566,664	131,904,618,362	80.0
064	Ministry of Agriculture, Livestock Development and Fisheries - Fisheries Sector	16,417,171,549	12,945,832,876	78.9
065	Prime Minister's Office - Labour, Youth Development, Employment and Dissabilities	15,627,581,654	14,575,160,817	93.3
066	Planning Commission	4,936,364,000	3,913,426,797	79.3
067	Public Service Recruitment Secretariat	2,481,424,144	2,224,179,756	89.6
068	Ministry of Works, Transport and Communication - Communication	4,517,800,600	3,689,334,822	81.7
069	Ministry of Natural Resources and Tourism	97,211,868,209	61,039,688,338	62.8
070	RAS Arusha	216,025,379,959	177,092,090,074	82.0
071	RAS Pwani	170,948,948,425	146,226,628,755	85.5
072	RAS Dodoma	208,324,876,132	155,467,292,568	74.6
073	RAS Iringa	152,999,339,000	120,466,864,263	78.7
074	RAS Kigoma	159,941,718,840	123,606,917,666	77.3
075	RAS Kilimanjaro	245,171,873,543	194,009,356,688	79.1
076	RAS Lindi	112,158,640,220	85,652,405,388	76.4
077	RAS Mara	214,760,967,216	164,826,406,820	76.7
078	RAS Mbeya	228,241,768,251	184,510,305,242	80.8
079	RAS Morogoro	264,229,004,179	210,576,271,711	79.7
080	RAS Mtwara	150,980,231,593	115,017,230,232	76.2
081	RAS Mwanza	289,295,772,005	235,761,340,676	81.5
082	RAS Ruvuma	174,151,342,542	138,448,578,717	79.5
083	RAS Shinyanga	142,118,591,000	112,360,402,073	79.1
084	RAS Singida	138,787,598,329	105,381,556,946	75.9
085	RAS Tabora	182,025,741,767	143,529,018,889	78.9
086	RAS Tanga	261,578,463,000	206,727,352,608	79.0
087	RAS Kagera	215,588,783,034	172,391,523,996	80.0
088	RAS Dar Es Salaam	418,753,128,202	285,018,424,092	68.1
089	RAS Rukwa	96,270,500,574	80,028,961,394	83.1
090	RAS Songwe	89,777,316,000	69,622,747,496	77.6
091	Drug Control and Enforcement Authority	4,269,245,230	3,993,891,900	93.6
092	Tanzania Commission for AIDS (TACAIDS)	2,556,974,050	2,205,317,110	86.2
093	Immigration Department	50,979,329,600	43,407,401,241	85.1
094	Public Service Commission	6,280,902,348	5,546,059,888	88.3
095	RAS Manyara	151,470,794,000	128,734,310,481	85.0
096	Ministry of Information, Culture, Arts and Sports	27,803,352,312	23,005,580,903	82.7
098	Ministry of Works, Transport and Communication - Works	35,565,163,331	34,756,637,902	97.7
099	Ministry of Agriculture - Livestock Development	33,448,698,384	30,443,617,532	91.0
	TOTAL	**20,279,316,043,552**	**18,778,474,769,661**	**92.6**

B. MATUMIZI YA MAENDELEO

Vote Code	Vote Description	Revised Budget	Total Actual Expenditure	Actual Exp. As A % Of Annual Exp. Targets
MATUMIZI YA MAENDELEO KWA FEDHA ZA NDANI				
004	Archives Management Department	2,000,000,000	1,844,832,512	92.2
005	National Irrigation Commission	5,600,000,000	1,539,466,296	27.5
007	Treasury Registrar	1,000,000,000	-	-
014	Fire and Rescue	3,500,000,000	12,754,650	0.4
021	The Treasury	266,225,423,111	259,700,000,000	97.5
023	Accountant General's Department	2,000,000,000	903,280,343	45.2
028	Ministry of Home Affairs - Police Force	5,000,000,000	-	-
029	Ministry of Home Affairs - Prisons Services	7,200,000,000	5,000,000,000	69.4
030	President's Office and Cabinet Secretariat	54,987,317,517	2,184,728,300	4.0
031	Vice President's Office	2,665,546,000	1,325,796,100	49.7
032	President's Office - Public Service Management and Good Governance	7,000,000,000	6,755,792,173	96.5
033	Ethics Secretariat	2,300,000	-	-
034	Ministry of Foreign Affairs	8,000,000,000	3,420,195,655	42.8
036	RAS Katavi	19,053,248,000	9,178,845,761	48.2
037	Prime Minister's Office	6,000,000,000	4,023,623,100	67.1
038	Defence	10,000,000,000	10,000,000,000	100.0
039	National Service	6,000,000,000	1,000,000,000	16.7
040	Judiciary Fund	18,358,131,000	10,779,003,000	58.7
041	Ministry of Constitutional Affairs and Justice	994,115,000	481,999,999	48.5
042	The National Assembly Fund	7,000,000,000	3,681,424,626	52.6
043	Ministry of Agriculture,Livestock and Fisheries-Agriculture Sector	50,672,368,373	25,717,400,260	50.8
044	Ministry of Industry, Trade and Investment	73,575,068,000	13,600,347,094	18.5
045	National Audit Office	8,130,000,000	1,029,097,742	12.7
046	Ministry of Education, Science and Tehcnology	622,519,172,674	537,541,529,406	86.3
047	RAS Simiyu	27,999,074,000	11,551,994,754	41.3
048	Ministry of Lands,Housing and Human Settlements Development	16,400,000,000	4,043,608,901	24.7
049	Ministry of Water and Irrigation	404,678,686,447	190,759,332,036	47.1
050	Ministry of Finance and Planning	3,500,000,000	475,512,618	13.6
051	Ministry of Home Affairs	20,000,000,000	20,000,000,000	100.0
052	Ministry of Health, Community Development, Gender, Elderly and Children - Health	176,300,000,000	100,746,079,206	57.1
053	Ministry of Health, Community Development, Gender, Elderly and Children	2,000,000,000	-	-
054	RAS Njombe	20,939,290,000	10,722,690,565	51.2
056	President's Office - Regional Administration and Local Government Authorities	308,314,910,000	254,674,892,828	82.6
057	Ministry of Defence and National Service	206,187,399,353	206,187,393,353	100.0
058	Ministry of Energy and Minerals	772,797,285,647	532,832,415,606	68.9
060	Trade and Investment	9,376,341,090	4,026,341,090	42.9
061	Electoral Commission	10,000,000,000	3,295,617,840	33.0
062	Ministry of Works, Transport and Communication - Tansport	1,890,853,184,620	528,228,525,090	27.9
063	RAS Geita	30,568,207,000	16,609,424,989	54.3
064	Ministry of Agriculture, Livestock Development and Fisheries - Fisheries Sector	-	-	-
065	Prime Minister's Office - Labour, Youth Development, Employment and Dissabilities	16,000,000,000	3,047,000,295	19.0
066	Planning Commission	4,475,800,000	636,742,289	14.2
067	Public Service Recruitment Secretariat	750,000,000	-	-
068	Ministry of Works, Transport and Communication - Communication	14,000,000,000	2,589,395,223	18.5
069	Ministry of Natural Resources and Tourism	34,803,284,000	-	-
070	RAS Arusha	47,279,528,000	22,105,575,209	46.8
071	RAS Pwani	43,474,536,000	21,361,922,697	49.1
072	RAS Dodoma	39,359,823,000	16,772,523,858	42.6
073	RAS Iringa	27,348,004,000	12,899,039,397	47.2
074	RAS Kigoma	32,947,898,000	14,684,603,379	44.6
075	RAS Kilimanjaro	36,310,689,000	17,954,496,043	49.4
076	RAS Lindi	21,646,572,614	6,688,308,263	30.9
077	RAS Mara	36,873,583,000	18,509,855,963	50.2
078	RAS Mbeya	39,979,111,000	13,470,501,118	33.7
079	RAS Morogoro	43,880,160,000	18,196,394,218	41.5
080	RAS Mtwara	40,513,398,000	15,322,058,868	37.8
081	RAS Mwanza	53,783,623,000	22,114,816,598	41.1
082	RAS Ruvuma	37,923,017,000	16,348,014,642	43.1
083	RAS Shinyanga	31,612,469,000	10,427,444,134	33.0
084	RAS Singida	29,091,179,965	17,910,145,730	61.6
085	RAS Tabora	39,278,829,000	13,973,335,102	35.6
086	RAS Tanga	48,952,701,903	18,733,973,095	38.3
087	RAS Kagera	35,991,248,000	16,438,550,561	45.7
088	RAS Dar Es Salaam	293,009,416,000	31,071,637,626	10.6
089	RAS Rukwa	17,809,080,000	9,646,527,579	54.2
090	RAS Songwe	25,527,205,000	16,439,264,498	64.4
092	Tanzania Commission for AIDS (TACAIDS)	3,000,000,000	-	-
093	Immigration Department	4,000,000,000	3,158,000,000	79.0
095	RAS Manyara	31,747,547,000	15,690,241,121	49.4
096	Ministry of Information, Culture, Arts and Sports	6,320,000,000	3,870,947,528	61.2
098	Ministry of Works, Transport and Communication-Works	1,950,076,695,332	1,904,875,419,456	97.7
099	Ministry of Agriculture,Livestock and Fisheries	3,986,000,000	-	-
	SUB TOTAL	**8,179,148,465,645**	**5,068,810,680,383**	**62.0**

MATUMIZI YA MAENDELEO KWA FEDHA ZA NJE				
005	National Irrigation Commission	14,503,412,150	2,468,251,364	17.0
007	Treasury Registrar	1,000,000,000	597,411,183	59.7
021	The Treasury	41,447,143,617	32,866,342,973	79.3
023	Accountant General's Department	1,600,000,000	1,357,793,500	84.9
028	Ministry of Home Affairs - Police Force	253,623,000	-	-
029	Ministry of Home Affairs - Prisons Services	54,742,000	-	-
030	President's Office and Cabinet Secretariat	365,070,890,000	10,949,761,437	3.0
031	Vice President's Office	4,122,906,437	2,084,576,358	50.6
032	President's Office - Public Service Management and Good Governance	-	230,000	-
033	Ethics Secretariat	1,647,700,000	558,160,061	33.9
036	RAS Katavi	9,882,412,360	9,794,165,657	99.1
037	Prime Minister's Office	60,165,372,763	44,404,974,548	73.8
040	Judiciary Fund	92,000,842,312	14,289,232,242	15.5
041	Ministry of Constitutional Affairs and Justice	1,806,020,000	114,088,000	6.3
042	The National Assembly Fund	200,000,000	-	-
043	Ministry of Agriculture,Livestock and Fisheries-Agriculture Sector	86,328,319,700	1,292,792,725	1.5
044	Ministry of Industry, Trade and Investment	265,309,000	-	-
045	National Audit Office	3,670,948,000	1,499,910,000	40.9
046	Ministry of Education, Science and Tehcnology	294,322,649,326	175,443,751,807	59.6
047	RAS Simiyu	21,954,950,459	16,427,454,094	74.8
048	Ministry of Lands,Housing and Human Settlements Development	9,000,000,000	8,999,999,999	100.0
049	Ministry of Water and Irrigation	214,418,125,839	151,507,953,372	70.7
050	Ministry of Finance and Planning	12,450,680,300	6,139,125,865	49.3
052	Ministry of Health, Community Development, Gender, Elderly and Children - Health	450,012,291,020	225,646,655,979	50.1
053	Ministry of Health, Community Development, Gender, Elderly and Children	606,278,000	-	-
054	RAS Njombe	16,065,466,733	11,195,611,061	69.7
055	Commission for Human Rights and Good Governance	2,272,796,000	76,737,680	3.4
056	President's Office - Regional Administration and Local Government Authorities	124,342,933,045	102,330,284,583	82.3
058	Ministry of Energy and Minerals	164,627,327,000	12,654,822,266	7.7
062	Ministry of Works, Transport and Communication - Tansport	250,285,183,000	-	-
063	RAS Geita	20,344,604,574	17,741,909,228	87.2
064	Fisheries Sector	2,000,000,000	2,000,000,000	100.0
065	Prime Minister's Office - Labour, Youth Development, Employment and Dissabilities	1,400,000,000	484,210,359	34.6
069	Ministry of Natural Resources and Tourism	17,000,000,000	3,486,925,320	20.5
070	RAS Arusha	10,545,695,059	8,309,847,230	78.8
071	RAS Pwani	16,261,218,394	15,614,315,798	96.0
072	RAS Dodoma	13,153,588,626	11,624,753,325	88.4
073	RAS Iringa	16,609,635,152	11,938,645,204	71.9
074	RAS Kigoma	13,919,366,786	11,008,227,084	79.1
075	RAS Kilimanjaro	18,328,333,507	15,062,154,898	82.2
076	RAS Lindi	15,089,545,989	13,313,590,455	88.2
077	RAS Mara	17,696,476,038	15,925,356,781	90.0
078	RAS Mbeya	13,015,838,000	7,776,506,569	59.7
079	RAS Morogoro	27,006,671,126	24,258,983,878	89.8
080	RAS Mtwara	10,782,628,999	6,147,525,468	57.0
081	RAS Mwanza	17,120,267,489	13,167,146,127	76.9
082	RAS Ruvuma	25,197,367,210	17,446,004,142	69.2
083	RAS Shinyanga	20,707,817,402	19,999,090,287	96.6
084	RAS Singida	15,623,257,250	15,217,179,872	97.4
085	RAS Tabora	27,794,794,700	23,629,369,521	85.0
086	RAS Tanga	14,282,057,245	13,236,651,441	92.7
087	RAS Kagera	22,169,781,536	19,172,832,911	86.5
088	RAS Dar Es Salaam	95,036,583,865	9,343,524,771	9.8
089	RAS Rukwa	17,071,198,530	13,860,105,763	81.2
090	RAS Songwe	7,713,319,000	4,980,957,289	64.6
092	Tanzania Commission for AIDS (TACAIDS)	6,514,259,869	116,610,000	1.8
095	RAS Manyara	12,259,266,760	10,626,965,679	86.7
098	Ministry of Works, Transport and Communication-Works	514,485,479,636	316,198,557,122	61.5
099	Ministry of Agriculture,Livestock and Fisheries	14,000,000	1,030,000	7.4
	SUB TOTAL	**3,253,521,374,804**	**1,474,389,063,274**	**45.3**
	GRAND TOTAL (DEVELOPMENT LOCAL + DEVELOPMENT FOREIGN)	**11,432,669,840,448**	**6,543,199,743,657**	**57.2**

SEHEMU YA PILI

MWONGOZO WA MAANDALIZI YA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2019/20 – 2021/22

UTANGULIZI

113. Mwongozo wa Mpango na Bajeti (Mwongozo) unatoa maelekezo kwa Maafisa Masuuli wa Wizara, Idara Zinazojitegemea, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Taasisi na Mashirika ya Umma kuhusu uandaaji wa maoteo ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2019/20 pamoja na miaka miwili inayofuata. Mwongozo wa Mpango na Bajeti umeandaliwa kwa mujibu wa Kifungu Na. 21 cha Sheria ya Bajeti Na. 11 ya Mwaka 2015. Hivyo, Maafisa Masuuli wanatakiwa kuzingatia maelekezo yaliyotolewa kwenye Mwongozo katika kuandaa Mipango ya Muda wa Kati na Bajeti ikijumuisha taarifa za utekelezaji kama ilivyoainishwa katika Sura ya pili.

114. Lengo kuu la kuandaa Mpango wa Muda wa Kati na Bajeti (2019/20 hadi 2021/22) ni kuhakikisha ufanisi katika ukusanyaji wa mapato, nidhamu katika matumizi, utengaji na ugawaji wa rasilimali kimkakati. Maafisa Masuuli wanatakiwa kuzingatia uhalisia wa makadirio ya mapato na matumizi kwenye Mfumo wa Muda wa Kati wa Mapato na Matumizi (MTEF) kwa kutenga makadirio halisia ya mapato na matumizi kwa mwaka 2019/20 na miaka miwili inayofuata (2020/21 na 2021/22).

115. Katika kuandaa mipango na bajeti, Maafisa Masuuli wanaelekezwa kuzingatia Sera na Miongozo ifuatayo: Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, 2016/17 – 2020/21 (FYDP II); Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2015; Sheria ya Bajeti, SURA 439 pamoja na Kanuni zake; Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa Awamu ya Tatu; Malengo Endelevu ya Maendeleo (SDGs); Mwongozo wa Ushirikiano wa Kimaendeleo (DCF); sanjari na makubaliano mengine ya kikanda na Kimataifa ambayo Serikali imeyaridhia.

116. Mwongozo umegawanyika katika sura mbili. Sura ya Kwanza inatoa maelekezo ya kuzingatia katika kuandaa mipango ya muda wa kati na bajeti (2019/20 – 2021/22); na Sura ya Pili inaainisha namna ya ujazaji wa fomu na utoaji wa taarifa za utekelezaji wa mipango ya muda wa kati na bajeti. Mwongozo huu utasomwa kwa pamoja na Juzuu I ya Sera na Mfumo wa Bajeti katika kipindi cha Muda wa Kati.

SURA YA KWANZA

MWONGOZO WA MAANDALIZI YA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2019/20 – 2021/22

1.1. Mfumo wa Mapato na Matumizi

117. Mfumo wa mapato na matumizi unaainisha makadirio ya mapato na matumizi kwa maeneo makuu ambayo ni Kodi, Maduhuli, Misaada, Mikopo, Mishahara, Matumizi Mengineyo, Deni la Taifa na Matumizi ya Maendeleo. Maelezo ya ziada ya sera za mapato na matumizi yanapatikana katika sura ya tatu ya Juzuu I ya Sera na Mfumo wa Bajeti katika kipindi cha Muda wa Kati.

1.1.1. Mapato ya Serikali

118. Mapato ya Serikali yanatarajiwa kuongezeka katika kipindi cha muda wa kati (2019/20 – 2021/22). Mapato yanakadiriwa kufikia kiasi cha Shilingi bilioni 33,500.2 (sawa na asilimia 21.1 ya Pato la Taifa) katika mwaka 2019/20 na kuongezeka kufikia shilingi bilioni 35,749.6 (sawa na asilimia 20.6 ya Pato la Taifa) kwa mwaka 2020/21 na Shilingi bilioni 38,172.5 (sawa na asilimia 20.2 ya Pato la Taifa) kwa mwaka 2021/22.

119. Katika mwaka 2019/20, Serikali inatarajia kukusanya mapato ya shilingi bilioni 33,500.2, ambapo mapato ya kodi yanakadiriwa kuwa Shilingi bilioni 20,124.1, maduhuli Shilingi bilioni 2,287.0, mapato ya ndani ya Mamlaka za Serikali za Mitaa Shilingi bilioni 795.7 na vyanzo vingine vitachangia Shilingi bilioni 10,293.3.

1.1.2. Matumizi ya Serikali

120. Katika muda wa kati (2019/20 – 2021/22), Serikali inatarajia kutumia shilingi bilioni 33,500.2 (sawa na asilimia 21.1 ya Pato la Taifa) kwa mwaka 2019/20 na kuongezeka kufikia Shilingi bilioni 35,749.6 (sawa na asilimia 20.6 ya Pato la Taifa) kwa mwaka 2020/21 na Shilingi bilioni 38,172.5 (sawa na asilimia 20.2 ya Pato la Taifa) kwa mwaka 2021/22.

121. Katika mwaka 2019/20, matumizi ya Serikali yanatarajiwa kuwa Shilingi bilioni 33,500.2 (sawa na asilimia 21.1 ya Pato la Taifa). Matumizi ya kawaida yanakadiriwa kufikia shilingi bilioni 21,115.8, sawa na asilimia 13.3 ya Pato la Taifa ambapo mishahara (ikijumuisha mishahara ya Taasisi na Mashirika ya Umma) inakadiriwa kufikia Shilingi bilioni 7,559.0, sawa na asilimia 4.8 ya Pato la Taifa, Huduma za Mfuko Mkuu wa Serikali Shilingi bilioni 10,376.1 (sawa na asilimia 6.5 ya Pato la Taifa) na matumizi mengineyo ni shilingi bilioni 3,180.7 (sawa na asilimia

2.0 ya Pato la Taifa). Matumizi ya maendeleo yanakadiriwa kuwa Shilingi bilioni 12,384.4, ikijumuisha Shilingi bilioni 9,555.7, fedha za ndani na Shilingi bilioni 2,828.7 fedha za nje. Kiwango hiki ni sawa na asilimia 37.0 ya bajeti ya mwaka 2019/20, sawa na asilimia 7.8 ya Pato la Taifa.

1.2. Uandaaji wa Mipango na Bajeti

122. Maafisa Masuuli wa Wizara, Idara Zinazojitegemea, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Taasisi na Mashirika ya Umma wanapaswa kuandaa na kukamilisha mipango na bajeti kwa wakati na kuwasilisha Wizara ya Fedha na Mipango kwa kuzingatia ratiba kama ilivyoainishwa katika Mwongozo.

1.2.1. Kamati za Bajeti

123. Kamati za Bajeti zimeanzishwa kwa mujibu wa Kifungu cha 18(2) cha Sheria ya Bajeti Na. 11 ya mwaka 2015. Kamati hizi zinatekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Kanuni ya 17(3) ya Kanuni za Bajeti za mwaka 2015. Maafisa Masuuli wanaelekezwa kuhakikisha kuwa Kamati za Bajeti zinatekeleza majukumu yake ipasavyo wakati wa uandaaji na utekelezaji wa mipango na bajeti. Vile vile, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Taasisi na Mashirika ya Umma pamoja na maelekezo hayo ya jumla, zinaelekezwa kuzingatia Nyaraka na maelekezo yanayotolewa na Ofisi ya Rais – TAMISEMI na Ofisi ya Msajili wa Hazina, mtawalia.

1.2.2. Ratiba ya Maandalizi ya Mipango na Bajeti

124. Wizara, Idara Zinazojitegemea, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Taasisi na Mashirika ya Umma zinaelekezwa kuandaa mipango na bajeti katika Mfumo wa Mapato na Matumizi wa Muda wa Kati (MTEF) na kuwasilisha Wizara ya Fedha na Mipango kwa ajili ya uchambuzi katika kipindi cha wiki ya kwanza ya mwezi Februari 2019.

125. Vile vile, Wizara, Idara Zinazojitegemea, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Taasisi na Mashirika ya Umma zinaelekezwa kupitisha mipango na bajeti zao kwenye mabaraza ya wafanyakazi kwa mujibu wa matakwa ya Sheria ya Majadiliano ya Pamoja katika Utumishi wa Umma SURA 105 wiki ya tatu ya mwezi Januari 2019.

1.2.3. Uchambuzi wa Mipango na Bajeti

126. Ili kuwa na ufanisi na kufikia malengo ya uchambuzi wa Mipango na Bajeti, Maafisa Masuuli wanatakiwa kuwasilisha Wizara ya Fedha na Mipango MTEF siku tano kabla ya tarehe ya uchambuzi kuwezesha wadau kupitia na kufanya uchambuzi wa kina ili kuboresha mipango na bajeti.

127. Uchambuzi wa makadirio ya mapato na matumizi kwa kipindi cha muda wa kati utafanywa na Wizara ya Fedha na Mipango kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora; Ofisi ya Rais- Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Ofisi ya Msajili wa Hazina. Wizara, Idara zinazojitegemea, Wakala za Serikali, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Taasisi na Mashirika ya Umma zinaelekezwa kuwasilisha nakala tano za rasimu ya MTEF pamoja na nakala laini kwa ajili ya uchambuzi. Baada ya uchambuzi na maboresho, Maafisa Masuuli wanatakiwa kuwasilisha nakala moja (1) kwa Wizara ya Fedha na Mipango, Ofisi ya Rais - TAMISEMI na Ofisi ya Msajili wa Hazina.

128. Katika kuhakikisha uhalisia wa mipango na makadirio ya mapato na matumizi, zoezi la uchambuzi litafanyika kwa kuzingatia yafuatayo: -

(i) Mapitio ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2017/18;
(ii) Mapitio ya mwenendo wa mapato na matumizi ya mwaka 2017/18 hadi kipindi cha nusu mwaka wa 2018/19 yakijumuisha changamoto na masuala msingi yaliyojitokeza wakati wa utekelezaji wa mipango na bajeti;
(iii) Muundo wa uwasilishaji wa MTEF kwa mwaka 2019/20 hadi 2021/22 kama ilivyoainishwa kwenye Sura ya Pili ya Mwongozo;
(iv) Mapitio ya utekelezaji wa mpango wa usimamizi vihatarishi kwa mwaka 2018/19 na mpango wa usimamizi vihatarishi kwa mwaka 2019/20 kama ilivyoainishwa katika Mwongozo wa Maandalizi na Utekelezaji wa Vihatarishi kwa Taasisi za Umma wa mwaka 2012/13;
(v) Vipaumbele vilivyoainishwa kwenye Mpango wa Pili wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (FYDP II);
(vi) Ukomo wa Bajeti wa Mifuko ya Pamoja ya Sekta (Basket funds) itaidhinishwa na kusambazwa na Wizara ya Fedha na Mipango peke yake;
(vii) Mwongozo wa Usimamizi wa Uwekezaji wa Umma wa Mwaka 2015 (PIM-OM) katika uandaaji wa miradi ya maendeleo;
(viii) Maelekezo ya Mwongozo, Sheria ya Bajeti Na. 11 ya mwaka 2015 na Kanuni za mwaka 2015, Nyaraka za Msajili wa Hazina pamoja na maelekezo mengine ya Serikali; na
(ix) Utumiaji sahihi wa GFS Codes.

129. Maafisa Masuuli wanaelekezwa kuwasilisha miradi mipya inayotarajia kuingizwa kwenye Bajeti ya Serikali ya mwaka 2019/20 wiki ya mwisho ya mwezi Januari, 2019. Miradi itakayowasilishwa baada ya Januari, 2019 haitaingizwa kwenye bajeti ya mwaka 2019/20 badala yake itazingatiwa kwenye bajeti ya mwaka

2020/21 na 2021/22.

1.2.4. Majumuisho ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali

130. Maafisa Masuuli wanatakiwa kuwasilisha Randama kwenye Kamati za Kudumu za Bunge za Kisekta kwa ajili ya uchambuzi na maboresho kuanzia wiki ya tatu ya mwezi Machi 2019 hadi wiki ya kwanza ya mwezi Aprili 2019. Baada ya uchambuzi wa Kamati za Kudumu za Bunge, Wizara ya Fedha na Mipango itafanya majumuisho ya makadirio ya mapato na matumizi kwa Mafungu yote na kuwasilishwa kwa ridhaa katika ngazi mbalimbali za Serikali na idhini ya Bunge la Jamhuri ya Muungano kuanzia wiki ya pili ya mwezi Aprili 2019 hadi wiki ya nne ya mwezi Juni 2019.

1.2.5. Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi-PPP

131. Maafisa Masuuli wanatakiwa kuzingatia utaratibu wa ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi (PPP) kama njia mojawapo ya kutekeleza miradi ya maendeleo kwa kuzingatia Sheria ya Ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi Sura ya 103. Kwa hiyo, wakati maandalizi ya bajeti yanaanza, Maafisa Masuuli wanatakiwa kuchambua na kuainisha miradi yenye sifa za kutekelezwa kwa utaratibu wa PPP na kuiwasilisha Wizara ya Fedha na Mipango kulingana na hitaji la Sheria ya PPP. Taasisi za Serikali zenye miradi yenye sifa za kutekelezwa kwa utaratibu wa PPP zinatakiwa kukamilisha upembuzi yakinifu na kuwasilisha Wizara ya Fedha na Mipango kwa uidhinishwaji au kupatiwa mapendekezo kabla ya kuingia mikataba husika. Mamlaka za Serikali za Mitaa zitaandaa na kuwasilisha miradi ya ubia Ofisi ya Rais - TAMISEMI kwa uchambuzi na kupata mwongozo wa utekelezaji wake.

132. Uidhinishaji wa fedha za kuandaa upembuzi yakinifu na utekelezaji wa miradi ya PPP utazingatia kikamilifu Sheria ya PPP ikiwa ni pamoja na uchambuzi wa mradi husika kuonesha kuwa utekelezaji wake kupitia utaratibu wa PPP una tija na thamani ya fedha zaidi kulinganisha na utekelezaji wa mradi kupitia bajeti ya Serikali.

1.2.6. Uingizaji wa Takwimu za Bajeti ya Serikali kwenye Mifumo ya CBMS na PlanRep

133. Maafisa Masuuli wanaelekezwa kukamilisha uingizaji takwimu za bajeti kwa usahihi na kuzingatia muda kwenye Mifumo ya CBMS na PlanRep kwa kuzingatia yafuatayo:

(i) Uhalisia wa makadirio ya mapato na matumizi ya mwaka 2019/20 na makisio ya miaka miwili inayofuata (2020/21 na 2021/22);

(ii) Matumizi sahihi ya Government Finance Statistics (GFS) 2014 na namba za

miradi zinazotolewa na Wizara ya Fedha na Mipango;

(iii) Matumizi sahihi ya vizio vya vipimo kama vilivyoainishwa kwenye mifumo ya CBMS na PlanRep; na

(iv) Utengaji wa gharama halisi za pango, umeme, simu, maji na posho kwa kuzingatia miongozo inayotolewa na Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na Mlipaji Mkuu wa Serikali.

1.3. Mambo Mengine ya Kuzingatiwa katika Uandaaji wa Mipango na Bajeti

(a) Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa Awamu ya Tatu

134. Serikali itaendelea kutekeleza awamu ya tatu ya Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa pamoja na Mpangokazi wake (2017-2022). Serikali imetoa mafunzo ya namna ya kuandaa mpangokazi kwa Kamati za Maadili za Wizara zote na Sekretarieti za Mikoa 16 na Halmashauri husika. Utekelezaji wa awamu ya tatu ya Mkakati huu utalenga katika kupunguza na kudhibiti rushwa katika sekta/maeneo ya kimkakati ikijumuisha Ununuzi wa umma, Ukusanyaji wa Mapato, utoaji Haki, Maliasili na Utalii, Madini, Nishati, Mafuta na Gesi, Afya, Elimu na Ardhi. Taasisi zitakazopewa kipaumbele katika utekelezaji wa Mkakati ni Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Polisi, Mahakama, Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA), Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA), Afya na Elimu. Lengo kuu la Mkakati ni kuhakikisha kuwa rushwa inapungua kwa kuchukua hatua za kuzuia na kupambana na rushwa. Maafisa Masuuli wanaelekezwa kuzingatia yafuatayo:

(i) Kuimarisha ufanisi, uwazi na uwajibikaji katika utoaji wa huduma kwa sekta ya umma na binafsi;

(ii) Kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa mikakati ya kupambana na rushwa;

(iii) Kuzijengea uwezo Taasisi zinazohusika katika usimamizi wa mapambano dhidi ya rushwa;

(iv) Kuwa kinara na kujenga utamaduni wa kupambana na rushwa miongoni mwa viongozi wa kisiasa na jamii kwa ujumla; na

(v) Kuhakikisha kuwa mpangokazi wa kupambana na rushwa unatengewa fedha za utekelezaji wa mkakati.

(b) Matumizi ya Mfumo wa Serikali wa Kielektroniki wa Ukusanyaji wa Mapato na Malipo Mtandao (GePG)

135. Ili kupunguza uvujaji wa mapato ya Serikali na kuimarisha mfumo wa ufuatiliaji wa makusanyo ya mapato papo kwa hapo kwa mamlaka husika, Maafisa Masuuli wanaelekezwa kuzingatia yafuatayo:

(i) Kuweka mazingira wezeshi kwa ajili ya utumiaji na uendeshaji wa GePG;

(ii) Kuunganisha mifumo ya Ankara za malipo ya Taasisi zinazokusanya maduhuli na GePG; na

(iii) Kusimamia usalama na kuhakikisha GePG inakuwa endelevu.

(c) Miradi ya Kimkakati ya Kuongeza Mapato kwa Halmashauri (SGRP)

136. Serikali itaendelea kugharamia miradi ya Kimkakati ili kuongeza mapato ya ndani na kuboresha utoaji huduma katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Hivyo, Maafisa Masuuli wanaelekezwa kuzingatia yafuatayo:

(i) Kuendelea kuainisha, kupembua na kuwasilisha miradi ya Kimkakati Wizara ya Fedha na Mipango kupitia Ofisi ya Rais TAMISEMI kama ilivyoelekezwa kwenye mwongozo wa miradi ya kimkakati;

(ii) Maandiko ya Miradi ya kimkakati yatawasilishwa OR TAMISEMI kwa ajili ya uchambuzi wa awali kabla ya kuwasilishwa Wizara ya Fedha na Mipango;

(iii) Kutoa miongozo ya kuanisha maeneo ya kuanzisha miradi ya Kimkakati katika maeneo ya utawala husika ili kupunguza uwezekano wa miradi ya aina moja kuwekwa kwenye maeneo ya jirani na kuondoa ushindani katika upatikanaji wa malighafi na wateja na kuleta utengemafu baina ya miradi; na

(iv) Kuwasilisha taarifa za utekelezaji wa miradi ya kimkakati kama ilivyoainishwa kwenye Mwongozo wa Miradi ya Kimkakati.

(d) Hatua za Kudhibiti Matumizi

137. Maafisa Masuuli wanapaswa kusimamia nidhamu ya matumizi ya Fedha za Umma katika mamlaka husika kama ilivyoidhinishwa na Bunge. Vile vile, hatua za kudhibiti matumizi zitumike bila kuathiri ubora wa utoaji huduma katika maeneo yafuatayo: -

(i) Kuhakikisha thamani halisi ya fedha inazingatiwa katika ununuzi wa bidhaa, huduma na kandarasi za ujenzi kwa kuzingatia misingi ya kanuni za ununuzi wa umma kama *Force Account*, ununuzi wa pamoja na ushindanishaji Wazabuni;

(ii) Kuendelea na utaratibu wa kutumia Wakala ya Huduma za Ununuzi Serikalini kwenye ununuzi wa magari baada ya kupata kibali kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu;

(iii) Matumizi ya TEHAMA katika mawasiliano Serikalini kama vile matumizi ya majalada ya kielektroniki kwa lengo la kupunguza gharama na kuongeza ufanisi;

(iv) Safari za nje na gharama zisizo na tija;

(v) Kutumia kumbi za Taasisi za Umma kwa semina, mafunzo, warsha na mikutano ya Bodi;

(vi) Taasisi za umma zinaelekezwa kutumia Hati za madai na mikataba ya watoa huduma wa ndani kuwa katika fedha za Kitanzania (Shillingi) ili kupunguza athari za mabadiliko ya viwango vya ubadilishaji fedha;

(vii) Kupunguza uagizaji wa bidhaa kutoka nje ya nchi hasa kwa bidhaa

zinazozalishwa na viwanda vya ndani; na

(viii) Kutumia vifaa vya teknolojia vinavyopunguza matumizi ya nishati.

(e) Matumizi Maalum

138. Katika mwaka wa fedha wa 2018/19, Serikali ilianzisha vifungu mahsusi kuwezesha Wizara, Idara Zinazojitegemea, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Taasisi za Umma kutenga fedha kwa ajili ya madeni ya Wakandarasi, madeni ya Watumishi wa Umma na kifungu kwa watumishi wenye mahitaji maalum katika Utumishi wa Umma. Hivyo, Maafisa Masuuli wanaelekezwa kutumia vifungu hivi katika maandalizi ya mipango ya muda wa kati na Bajeti kama ilivyoainishwa katika mfumo wa *GFS codes* zifuatazo:

(i) 21113132 *Staff debts*

(ii) 22032122 *Suppliers debt*

(iii) 27210109 *Assistance to persons with disability*

(f) Ulipaji na Udhibiti wa Ulimbikizaji wa Madeni

139. Ili kudhibiti ulimbikizaji wa madeni, Maafisa Masuuli wanaelekezwa kuzingatia kifungu cha 52(1) cha Sheria ya Bajeti Na.11 ya Mwaka 2015. Hivyo, wanaelekezwa: -:

(i) Kuhakikisha madeni yote yamehakikiwa na Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Serikali;

(ii) Kuweka kipaumbele katika utengaji wa fedha za kulipia madeni yaliyohakikiwa kwa kutumia ukomo wa bajeti uliotolewa;

(iii) Kuhakikisha hakuna ulimbikizaji wa madeni mapya; na

(iv) Kuhakikisha miradi inayoendelea inajumuishwa kwenye mipango ya muda wa kati na bajeti kabla ya kujumuisha miradi mipya.

(g) Madeni Sanjari

140. Taasisi za umma zenye uhitaji wa mikopo kuhakikisha zinapata kibali kutoka kwa Waziri wa Fedha na Mipango kama ilivyoainishwa katika Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada kwa Serikali, SURA 134 kama ilivyorekebishwa mwaka 2004 pamoja na Kifungu cha 60(4) na 62(b) cha Sheria ya Bajeti Na. 11 ya mwaka 2015. Maafisa Masuuli wanaelekezwa kufuatilia kwa ukaribu mikataba yenye dhamana ili kuepuka madeni sanjari.

(h) Kiwango cha Ubadilishaji Fedha

141. Katika kuandaa Mpango na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2019/20, kiwango elekezi cha ubadilishaji fedha kitakachotumika kuthaminisha fedha za kigeni kwa Shilingi za Tanzania itakuwa Dola moja ya Marekani kwa Shilingi za Tanzania 2,316.40.

(i) Kujumuisha Masuala mtambuka katika Mipango na Bajeti

142. Maafisa Masuuli wanaelekezwa kujumuisha masuala mtambuka katika mipango na bajeti kama vile jinsia, ukimwi, watu wenye mahitaji maalum, lishe, mazingira, mabadiliko ya tabianchi na Utawala Bora.

(j) Usimamizi wa Taasisi na Mashirika ya Umma

143. Lengo kuu la Serikali katika kufanya maboresho ya utendaji na usimamizi wa Taasisi na Mashirika ya Umma ni pamoja na: kuongeza ufanisi na tija, kuboresha utoaji wa huduma na kuongeza faida; na kuongeza mchango katika Mfuko Mkuu wa Serikali. Msajili wa Hazina kwa kushirikiana na Wizara Mama wanaelekezwa kutekeleza yafuatayo: -

(i) Kuhakikisha kuwa Mashirika ya umma yanachangia asilimia 15 ya mapato ghafi katika Mfuko Mkuu wa Serikali kwa mujibu wa Sheria ya Msajili wa Hazina (Madaraka na Majukumu), SURA 370 ikijumuisha ziada kwa wakati;

(ii) Kuimarisha Mfumo wa ufuatiliaji wa Hisa za Serikali katika kampuni ambazo Serikali ina hisa chache;

(iii) Kuhakikisha Mashirika ya Umma yanayojiendesha kibiashara yanaandaa Mwongozo wa Gawio utakaotoa utaratibu wa malipo ya gawio kwa Serikali;

(iv) Kuteua wawakilishi wa Bodi na Watendaji wenye sifa na uwezo ili kuongeza tija na ufanisi katika utendaji wa Taasisi na Mashirika ya Umma;

(v) Kuchambua taarifa za fedha na mwenendo wa Taasisi na Mashirika ya Umma na kupendekeza hatua stahiki za kuboresha, kuunganisha au kufuta kwenye daftari la Msajili wa Hazina; na

(vi) Kufuatilia viwanda na mashamba yaliyobinafsishwa ili kubaini kama yanajiendesha kadiri ya mikataba ya mauzo na kuchukua hatua stahiki ikiwa ni pamoja na kurejesha Serikalini mashamba na viwanda ambavyo Wamiliki watabainika kukiuka mikataba ya mauzo.

(k) Ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa

144. Serikali itaendelea kutekeleza mikataba iliyoridhiwa na itifaki za Kikanda, baina ya nchi na kimataifa. Ili kushiriki kikamilifu na kufaidika na ushirikiano wa kikanda, baina ya nchi na kimataifa; Wizara, Idara Zinazojitegemea, Taasisi na Mashirika ya Umma, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa wanaelekezwa kuzingatia yafuatayo: -

(i) Kufuata Mwongozo wa Ushirikiano wa Kimaendeleo (DCF);

(ii) Kuhakikisha masuala ya EAC, SADC na makubaliano mengine ya kikanda yanajumuishwa katika mipango na bajeti;

(iii) Kutumia fursa za kifedha zinazotokana na maridhiano ya Kikanda, baina ya nchi na Kimataifa; na

(iv) Kuwasilisha michango stahiki kwa ajili ya kuchangia Taasisi za Kimataifa na Kikanda kwa Wizara ya Fedha na Mipango kwa ajili ya kujumuishwa kwenye bajeti.

(l) Fedha za Nje

145. Serikali itaendelea kushirikiana na wadau wa maendeleo katika kutekeleza programu na miradi ya maendeleo. Hivyo, Maafisa Masuuli wanatakiwa kuzingatia maelekezo yafuatayo katika kuandaa mipango na bajeti zao za mwaka 2019/20 hadi 2021/22: -

(i) Kutumia vigezo sahihi katika kubuni, kuchagua, kupembua na kutathmini miradi kabla haijapata kibali cha kupata fedha kama ilivyoelekezwa katika Mwongozo wa Usimamizi wa Uwekezaji wa Umma (PIM-OM);

(ii) Kuhakikisha fedha zinatengwa kwa ajili ya mchango wa Serikali katika utekelezaji wa miradi ya pamoja;

(iii) Wizara zinazoratibu Mifuko ya Pamoja ya Kisekta na programu zinatakiwa kuwasilisha viwango vya ukomo wa bajeti kwa ajili ya mpango wa muda wa kati (2019/20 – 2021/22) kabla ya mwisho wa mwezi wa Januari 2019;

(iv) Mikataba inayostahili kupata msamaha wa kodi ianishe kipengele cha msamaha wa kodi kwenye mikataba;

(v) Mikataba ya Makubaliano kati ya Washirika wa Maendeleo na Wizara, Idara zinazojitegemea, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Taasisi na Mashirika ya Umma zitasainiwa baada ya kupata kibali kutoka Wizara ya Fedha na Mipango;

(vi) Wizara, Idara zinazojitegemea, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Taasisi na Mashirika ya Umma wanaelekezwa kutenga fedha kwa ajili ya miradi na programu zinazoendelea ikiwemo miradi inayotekelezwa kwa kupelekewa fedha moja kwa moja (D-Fund); na

(vii) Kutoa mrejesho Wizara ya Fedha na Mipango na kuhasibu kwa wakati matumizi ya fedha zinazopelekwa moja kwa moja kwenye miradi.

1.4. Maelekezo Mahususi kwa Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

1.4.1. Maelekezo kwa Sekretarieti za Mikoa

146. Wakati wa kipindi cha Maandalizi ya Makadirio ya Mipango ya Muda wa Kati na Bajeti (2019/20 hadi 2021/22), Sekretarieti za Mikoa zinapaswa kuzingatia yafuatayo: -

(i) Kusimamia na kudumisha masuala ya Ulinzi na Usalama katika maeneo ya Utawala;

(ii) Kuimarisha utawala bora na uwajibikaji katika maeneo ya utawala kwa

kufanya Vikao vya Ushauri vya Wilaya na Mkoa (DCC & RCC);

(iii) Kutambua maeneo ya mipaka na kuweka alama za mipaka ya Mikoa, Wilaya na Tarafa;

